**Kanuni** za fedha kuzibana kampuni za mikopo umiza

UKURASA 4



**Zuio** la RC matangazo ya misiba lazua jambo

UKURASA 5

ALHAMISI FEBRUARI 25, 2021 — AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 12

**Ujue mkaa mpya ulioingia sokoni kurithi nishati kuni na mkaa wake**



Ukurasa 13

TMDA yahamishia kampeni zake kusaka viwango vitakasa mikono



Ukurasa 14

**Jamii inavyohamasishwa dawa asili ili kuepuka maambukizi ya corona**

## Mahafali ya kwanza Baraza la Wauguzi tangu 1953 ikibeba ya kipekee ya uuguzi

• Bosi Mkuu wa Uuguzi awasilisha dozi



Wauguzi wahitimu waliokua katika mahafali yao, Kibaha mkoani Pwani. **PICHA: MTANDAO**

tambua wajibu wao katika utoaji wa huduma huku wakizingatia maadili ya taaluma zao.

"Kitendo hiki kilitakiwa kutekeleza kipindi kirefu kilichopita na ni vyema kikatekelezwa na taaluma zote za sekta ya afya nchini, ili kuwafanya wahitimu kuheshimu taaluma zao," anasema.

Katika kuboresha na kutekeleza majukumu ya Baraza la Wauguzi na Wakunga nchini, ziada amelitaka kuzingatia ubora wa stadi na maadili ya taaluma, ili kushuhudia mabadiliko makubwa ya ubora wa huduma za afya nchini.

"Tumeendelea kushuhudia changamoto nyingi za huduma zinazotolewa bila kuzingatia maadili ikiwa ni pamoja na kunyanyaswa wateja, natoa msisitizo tena kwa wanataaluma wote wa sekta ya afya zingatieni viapo vyenu," anasema Ziada.

Sellah amewahimiza viongozi katika ngazi za mikoa na hospitali za rufani, ambazo wamepewa mamlaka na Sheria ya Uuguzi na Ukunga ya Mwaka 2010, kuchukua hatua za awali, panapobainika kuna upungufu katika utoaji wa huduma.

"Tekelezeni majukumu yenu kwa haraka iwezekanavyo na kisha mtoe taarifa kwa Baraza la Uuguzi na Ukunga makao makuu kwa hatua zaidi.

"Wateja wanapenda kushuhudia haki inapatikana mapema, kuchelewa kuchukua hatua panapotokea upungufu kunaleta picha mbaya kwa wateja na kuleta taswira kuwa kuna kulindana au udhaifu katika usimamizi wa maamuzi,"anasema.

Ziada analipongeza baraza hilo kwa kuandaa tukio hilo na kuwahimiza liwe endelevu kwa wanataaluma kuelewa maana ya baraza na majukumu yake, pia akiwasisitiza kuhusu maadili ya taaluma yao.

Mwenyekiti wa Baraza la Uuguzi na Ukunga nchini, Abner Mathube, anasema sheria iliyounda baraza hilo ilitungwa kwa lengo la kuhakikisha Watanzania wanapata huduma za uuguzi na ukunga zilizo salama.

Hivyo, baraza hilo limechukua hatua ya kuhakikisha linawasajili wataalamu wenye sifa za kitaaluma na kuwachukulia hatua za kisheria, wote wanaotoa huduma chini ya viwango vilivyowekwa.

Wakati huo huo Kaimu Msajili wa Baraza la Uuguzi na Ukunga, Happy Masenga, anasema baraza linahakikisha leseni ya kutoa huduma za kitaaluma za uuguzi inatolewa kwa waombaji walioptia mafunzo yaliyokubalika, kutoka vyuo vinavyotambulika na kufaulu mitihani ya usajili inayoendeshwa na baraza.

Masenga anasema, tangu mwaka 2014, baraza hilo limekuwa likiendesha mitihani ya usajili na leseni, ili kupima umahiri wa wahitimu kwa lengo la kujiridhisha kama wanao uwezo wa kutoa huduma salama kwa wateja na hadi sasa wahitimu 30,715 wamekwishaifanya mitihani hiyo.

Ni mahafali yaliyoandaliwa na Baraza la Uuguzi na Ukunga nchini na yamefanyika kwa mara ya kwanza tangu baraza hilo kuanzishwa mwaka 1953.

Ndani ya hafla hiyo, kuna jumla ya wauguzi na wakunga 839 walihitimu masomo ya uuguzi na ukunga katika ngazi mbalimbali na kufaulu mitihani ya usajili na leseni iliyofanyika Novemba, 2020.


# Nipashe

Alhamisi Februari 25, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580502

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


# Magufuli akusudia kuvunja Jiji la Dar

• **Awapa** mtihani Waziri Jafo, Mkurugenzi... *Endelea ukurasa 2*





Mwonekano wa daraja la juu lililopewa jina la Kijazi (Kijazi Interchange), katika makutano ya barabara za Morogoro, Sam Nujoma na Mandela, jijini Dar es Salaam, baada ya Rais Dk. John Magufuli (Picha ndogo), kulifungua rasmi jana. Kulia kwa Rais ni Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara (TANROADS), Mhandisi Patrick Mfugale. **PICHA: IKULU**

## Serikali yataja mambo 10 ya kukabili magonjwa ambukizi

UK. 4

## Muhimbili kusimika mashine 4 kujifukiza

UKURASA 4

**MICHEZO** **SIMBA: TULISTAHILI USHINDI** UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

# ... Awapa mtihani Jafo na mkurugenzi

**Romana Mallya na Joseph Baltazar**

RAIS John Magufuli amekubali Kituo Kikuu cha Mabasi Mbezi Luis jijini Dar es Salaam kuitwa jina lake kwa masharti kwamba watendaji wahakikishe hakuna ukandamizaji wa wananchi wanyonge ambao mara zote anawatetea.

Akizindua kituo hicho jana, jijini humo, kilichojengwa kwa Sh. bilioni 50.95, Rais Magufuli alimtaka Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Suleiman Jafo, na Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam, kuhakikisha machinga hawafukuzwi kituoni.

Alisema kituo hicho kitahudumia mabasi 3,454 yakiwamo 1,000 yatakayolala na kina maegesho ya magari madogo 280 na kuagiza kuwapo pia maegesho ya bodaboda.

"Nimeshangaa Jafo kuandika stendi hii kwa jina langu kwa sababu angeandika Jafo Bus Stand, sifurahii majina yangu kutumika kwa sababu ninaogopa kitu kimoja mnaweza kuandika jina Magufuli halafu wananchi maskini, machinga wakawa wananyanyaswa hapa.

"Mara nyingi sina uhakika hapa, vitu vizuri vinavyotengenezwa vinapokamilika, machinga wanafukuzwa, watu wa kawaida wanafukuzwa, ndiyo maana nitaumia sana kama wananchi hawa wanyonge kufukuzwa halafu mmeandika jina Magufuli, maana yake Magufuli ndiye anawafukuza. Waziri inawezekana umejichongea kwa kuita stendi Magufuli, ninataka haya yafanyike," aliagiza.

Rais Magufuli alisema ndani ya stendi hiyo, kuna Ofisi ya Idara ya Uhamiaji, hoteli, nyumba za kulala wageni ambazo hana uhakika kama zitamgusa mmachinga.

"Nitoe wito waziri na mkurugenzi, mmenipa jina nimelikubali kwa ajili ya kuwatetea hawa watu. Ninataka niwe balozi wao kama mnataka hivyo. Ninataka stendi itapoanza, machinga wasifukuzwe kwa sababu ni kwao," aliagiza huku akishangiliwa.

Alisisitiza kuwa wasifukuzwe kwa sababu stendi hiyo kuna mabasi 3,000 ambapo abiria wanaotaka kununua chakula cha hoteli au machinga, wafanye hivyo. "Serikali ninayoiongoza, ni kwa ajili ya Watanzania wote hasa wanyonge. Watendaji mnaohusika, wananchi hawa waruhusiwe.

"Mtengeneze mbinu baadaye, mabasi yanapokuja, mtu anakimbia pale pembeni ananunua bidhaa zake, hapo ndipo tunapojenga Dar es Salaam yenye upendo, isiyokuwa na ubaguzi wa mtu yeyote.

Rais Magufuli alisema hataki kuona madalali wakiwadhulumu wananchi kwenye stendi hiyo na kumwagiza Waziri Jafo kulisimamia suala hilo.



Wananchi wakijipimia maeneo ya kufanya biashara nje ya kituo kikuu cha mabasi ya mikoani na nchi jirani cha Mbezi Luis, jijini Dar es Salaam jana, baada ya Rais Dk. John Magufuli kuutaka uongozi kutoa kipaumbele kwa wafanyabiashara wadogo, wakati akizindua kituo hicho. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# JPM kulivunja Jiji la Dar

**Na Romana Mallya**

RAIS John Magufuli ametangaza atalivunja Jiji la Dar es Salaam muda wowote kuanzia sasa na kulihamishia kwenye Manispaa ya Ilala, ili fedha zilizokuwa zinatumika, zielekezwe kwenye miradi ya maendeleo.

Alitangaza kusudio hilo jana, wakati wa hafla ya uzinduzi wa makutano ya barabara Ubungo jijini ambayo ujenzi wake umegharimu Sh. bilioni 252.642 huku Sh. bilioni 8.375 zikitumika kuwafidia wananchi waliopisha mradi huo.

Rais Magufuli alisema amekusudia kufanya mambo makubwa katika Jiji la Dar es Salaam, ili liwe na hadhi inayostahili.

"Kwa wana Dar es Salaam ninategemea kufanya mabadiliko kidogo ya kuwa na Manispaa ambazo zinawakilisha maeneo. Ninategemea kulivunja Jiji la Dar es Salaam, tutengeneze jiji la eneo fulani, tunaweza kuifanya Ilala kuwa jiji.

Rais Magufuli aliwataka wale waliokuwa wanataka nafasi ya Meya wa Jiji la Dar es Salaam, wajiandae kisaikolojia kwa sababu meya atapatikana Manispaa ya Ilala au manispaa mojawapo.

"Huu ndiyo kweli na rasimu nimeshaletewa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Suleman Jafo. Nikitoka hapa, nitakwenda kutia saini, ili turahisishe mambo.

"Bajeti ya Jiji ambayo haipo, fedha zilikuwa zinapotea, waheshimiwa wabunge, Ilala inafaa kuwa Jiji. Ubungo mtasubiri kwa sababu hata barabara hazijatengenezwa," alisema.

Rais Magufuli alisema anafanya hivyo kwa kuangalia matumizi mazuri ya fedha na kusisitiza lazima Dar es Salaam liwe jiji la kisasa.

"Kuwa na madiwani ambao wanakaa juu wanachangiwa fedha, wanakula posho, hili nitalikataza. Ninazungumza hapa, wale wanaojiandaa kuwa mameya wa Jiji la Dar es Salaam halafu wanakaa hawana maeneo, wajue hilo limekwisha," alisema.

Rais Magufuli alisema wanataka manispaa moja katika Jiji la Dar es Salaam ndiyo ipandishwe hadhi ya kuwa jiji kisha zingine zibaki kuwa manispaa.

Alisema wanafanya hivyo kama ilivyo kwenye majiji mengine na kutolea mfano Mwanza na Dodoma.

"Unapokuwa na manispaa nne au tano halafu unakuwa na madiwani hawawakilishi yoyote, wanawakilisha kwenye manispaa zao, halafu wanatengewa bajeti, hizo fedha ni vizuri zipelekwe kwenye miradi ya maendeleo ya barabara. Haya ndiyo matumizi bora ya fedha za walipakodi," alisema.

Rais alisema wamejipanga kuboresha maeneo mbalimbali ya jiji hilo na kuahidi wananchi wa mkoa huo wataona barabara nyingi za juu.

### DARAJA LA BALOZI KIJAZI

Rais Magufuli alipendekeza daraja hilo liitwe Balozi John Kijazi ambaye alikuwa Katibu Mkuu Kiongozi, aliyefariki dunia wiki iliyopita.

"Balozi Kijazi alifanya kazi kwa uadilifu na miradi yote ya Dar es Salaam ikiwamo masoko, stendi alikuwa Katibu Mkuu Kiongozi. Alikuwa kiongozi baraza na alichangia kwa kiasi kikubwa kufanikiwa kwa miradi mingi ikiwamo ya barabara.

"Ninafikiri wana Dar es Salaam, mtakubaliana nami Kijazi amefanya kazi kubwa sekta ya barabara, alikuwa hana makuu, alikuwa mkurugenzi wa barabara nchini, baada ya kutoka akateuliwa Mhandisi Patrick Mfugale (Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara (TANROADS).

"Baada ya Mfugale, akaja Alhaji Iyombe na baadaye akawa Katibu Mkuu na Kijazi akawa Katibu Mkuu, Mfugale ameumisi ukatibu mkuu kwa sababu hata umri hawezi kuteuliwa ukatibu," alisema.

Rais Magufuli alisema mchoraji wa madaraja likiwamo hilo la Ubungo ni Mfugale, akifafanua na kutania kidogo akisema:

"Ndiye mtaalamu wa madaraja. Alichora mchoro wa Daraja la Mkapa, Mfugale, Umoja, Busisi, ndiyo maana ninamwombea asife mapema au kujinyonga kwa sababu Wahehe wakishindwa mambo, wanajinyonga.

"Ninataka aendelee kuchora michoro ya madaraja mengine ili Dar es Salaam ibadilike."

Rais Magufuli alisema katika kipindi cha miaka 60, wanafahamu shida zilizokuwa Ubungo ambapo wapo waliopoteza maisha, ndoa kuvunjika kutokana na foleni iliyokuwapo.

"Wapo waliopoteza maisha yao, ninakumbuka mwaka 2015 wakati wa kampeni, Staff Sajenti alifia hapa kwenye mataa. Mungu aziweke roho za marehemu wote zilizotangulia kwa amani.

Alisema mwaka 2017, alifika hapo na Rais wa Benki ya Dunia (WB) kuweka jiwe la msingi na kwamba walifanya hivyo kwa sababu walihitaji fedha.

"Tungeweza kulijenga daraja, lakini kupanga ni kuchagua ukiwa unaaminika kwenye mikopo, ukikopeshwa na kulipa, Tanzania ni tajiri na matajiri wengi wanakopa na sisi matajiri Tanzania tukaenda kukopa Sh. bilioni 250 ambazo tutaanza kuzilipa," alisema.

Alisema wakati akitoka Posta kwenda Ubungo, alipita barabara ya Mwenge na ameshangaa kuona idadi kubwa ya nyumba za ghorofa Dar es Salaam, akisema sasa baadhi ya mitaa iliyopo inafanana na ya nchi za Ulaya.

Awali, Mfugale alisema kwa siku magari 68,800 yanapita katika makutano hayo na ili kuwezesha kupita, zamani yalikuwa yanatumia zaidi ya saa mbili na nusu kusubiriana.

"Daraja kutoka Kimara kwenda mjini lina urefu wa mita 260 ambalo linaruhusu gari kupita bila kusimama, limenyanyuliwa kwa mita 8.9 kutoka chini. Daraja kutoka Mwenge kwenda Buguruni limenyanyuliwa kwa mita 16.38 ambalo lina urefu wa mita 700," alifafanua.


**GSP AUCTION MART**

P.o.Box 31088 Dar es Salaam
Tanzania, Tel: + 255 687 638679 +255 654 922892
Sinza Africasana near by sokoni Africasana Block No. 31
Email: gsp.recovering@gmail.com / gsp.recovering@outlook.com

**KUMB No. TATA/2021/DM/019**

**GSP AUCTION MART** Kwa idhini na mamlaka tuliyopewa na kampuni ya ALLIANCE FINANCE CORPORATION LIMITED S.L.P 40780 Dar es salaam tunapenda kutangaza mnada wa hadhara wa kuuza Magari kwa njia ya mnada wa magari twaja hapo chini.Siku ya Ijumaa tarehe 05/03/2021 mnada utaanza Saa 5:00 kamili asubuhi katika yadi ya ALLIANCE FINANCE CORPORATION LIMITED iliyopo Dar es salaam vingunguti na Mwanza Sinai Mabatini.

| CUSTOMER NAME | MODEL | VEH_NO | LOCATION |
|---|---|---|---|
| MOSES PETER ABDONI | LP 909 BUS | T877DNN | DAR ES SALAAM |
| ABDALLAH KIBWANA KIBWANA | LP909 BUS | T351DPS | DAR ES SALAAM |
| ABADALLAH RAJABU TERRY | LPO 10.2T/52 | T323DME | DAR ES SALAAM |
| ABADALLAH RAJABU TERRY | LPO 10.2T/52 | T120DMK | DAR ES SALAAM |
| KAJORE OWIGO KITUGE | LPO 10.2T/52 | T430DQA | MWANZA |
| FRED MALI KAZI | XENON | T449DTV | MWANZA |

1. Dhamana itauzwa Kama ilivyo.
2. Mnunuzi anatakiwa kulipa siku hiyo hiyo ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14) kukamilisha malipo yote ukishindwa kufanya hivyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25% na mnada utarudiwa tena.
4. Gharama za kuona, kukaguwa, kuhamisha umiliki ni juu ya mnunuzi.
5. Kwa yeyote atakayeharibu mnada hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

**KWA TAARIFA ZAIDI WASILIANA NA:**
**GSP AUCTION MART PO BOX 310088 DAE ES SALAAM.**
**+255 654 922 892, +255 687 638 679**

## TANGAZO




# Benki ni SimBanking

Nunua Bima popote ulipo

PIGA
*150*03#
AU PAKUA MZIGO
App Store
Google Play

CRDB BANK
Tunakusikiliza

# Kanuni za fedha kuzibana kampuni za mikopo umiza

**Na Salome Kitomari,** MTWARA

KANUNI za huduma ndogo za fedha za mwaka 2018 za Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya mwaka 2017, zimeweka utaratibu unaowataka wakopeshaji binafsi, kampuni za mikopo na wakopeshaji kidigitali kuweka wazi masharti ya mikopo na viwango vya riba visivyo vya asilimia.

Watoa huduma hao ambao kwenye sheria ametajwa kama daraja la pili, wanatakiwa wawe wamesajiliwa chini ya Sheria ya Kampuni au sheria nyingine huku wakopeshaji binafsi watatakiwa kusajili jina chini ya sheria ya usajili wa majina ya biashara.

Watoa huduma hao watatakiwa kuwa na jina la mtoa huduma ndogo za fedha kujumuisha maneno ya 'Microfinance' au "Finance' au 'Financial' 'Services' au 'Credit' au 'Microcredit'.

Aidha, wakopeshaji hao wanatakiwa kuwa na sera ya mikopo kwa mujibu wa sheria, kuhakiki uwezo wa mkopaji na kulipa mkopo, kuwapo mkataba wa mikopo ambayo itaeleza wazi masharti ya mkopo husika na urejeshaji wake ikiwamo viwango vya riba kwa kiasi (tarakimu) na siyo asilimia na vilifafanuliwe kwa mwezi na mwaka.

"Kanuni inataka kuweka bayana vigezo na masharti ya mkopo ikiwamo kiasi cha mkopo, kiasi cha riba kwa mwaka, ada zote, riba halisi kwa mwaka, mpango wa malipo, kiasi chote cha fedha kitakachokuwa kimelipwa hadi mkataba wa mikopo uishe," alifafanua Meneja wa Huduma ndogo za fedha na maduka ya kubadilisha fedha za kigeni wa BoT, Victor Tarimu.

Kanuni hizo zimetaja kuwa ni lazima wawe na mtaji wa chini kabisa wa Sh. milioni 20, kiwango cha chini cha mali zenye ukwasi asilimia 15 ya mali zote, kufanyiwa ukaguzi na Benki Kuu ya Tanzania (BoT), uwasilishaji wa taarifa na BoT kuchukua umiliki wa mtoa huduma ndogo za fedha.

"Maombi yaambatane na ada ya Sh. 500,000 kwa kampuni na Sh. 300,000 kwa watu binafsi, pia benki itafanya tathmini ya uwezo wa kifedha, uzoefu, sifa na uadilifu wa wamiliki, wajumbe wa bodi na viongozi," alisema.

Aidha, watu binafsi wenye mikopo inayozidi Sh. milioni 20 au wateja au wanachama zaidi ya 100 watapaswa kuunda kampuni na kukidhi/ kuzingatia matakwa ya kampuni.

Kanuni hiyo imebainisha kuwa iwapo vigezo na masharti yote yametimizwa BoT itatoa leseni katika kipindi cha siku 60 baada ya kupokea maombi yaliyokamilika.

Pia ni lazima kuwe na Bodi ya Wakurugenzi au chombo cha usimamizi kwa kampuni, majukumu ya bodi na uongozi, biashara inayoruhusiwa na isiyoruhusiwa, matumizi ya dhamana ya fedha taslimu au amana ya kulazimishwa.

Mengine ni utunzaji wa hesabu na nyaraka zingine, uandaaji na uwekaji wazi mahesabu, vigezo vya ukaguzi wa ndani na wa nje na kuwasilisha taarifa katika taasisi ya taarifa za mikopo.

# Serikali yataja mambo 10 kukabili magonjwa ambukizi

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

SERIKALI imetaja hatua 10 za kukabiliana na magonjwa ya kuambukiza, ikiwamo Corona, huku ikiwataka viongozi kuacha kusubiri matamko zaidi, bali wawajibike kwa kuzingatia miongozo iliyopo.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, aliyasema jana alipokuwa akitoa tamko la kuongeza kasi ya utekelezaji wa hatua za kujikinga na magonjwa ya kuambukiza na yasiyoambukiza.

"Mheshimiwa Rais na Waziri Mkuu wameshafanya kazi kubwa na nzuri ya kutoa matamko ya kukumbusha na kuelimisha taifa juu ya mwelekeo wa tahadhari za kuchukua ili kuepuka mlipuko wa ugonjwa wa COVID-19, viongozi wa Wizara ya Afya tumetoa matamko mbalimbali ya kuwakumbusha na kuwaelimisha wananchi kuchukua tahadhari," alisema.

Alitaja hatua hizo za kuzingatiwa ni kuondoa hofu zinazojengwa bila sababu kwa kuwa zinasababisha madhara zaidi kiafya.

"Tuendeleze tabia ya kunawa mikono mara kwa mara kwa majisafi tiririka na sabuni. Iwapo maji tiririka na sabuni hakuna, tumia vipukusi (sanitizer)," alisema.

Alimwagiza Mfamasia Mkuu wa Serikali kuendelea kutoa elimu ya jinsi ya kutengeneza vipukusi vya ndani ya nchi ili wananchi wapate kwa bei nafuu.

"Vaa barakoa safi na salama ambayo umetengeneza mwenyewe au umenunua kwa watengenezaji wa ndani waliothibitishwa na Wizara ya Afya mfano Bohari ya Dawa, taasisi zetu za afya na watengenezaji wengine ambao tumewathibitisha," alisema.

Waziri huyo aliagiza Mfamasia Mkuu wa Serikali kutangaza orodha ya watengenezaji wa barakoa ambao wameshawathibitisha.

"Pia elimisha jinsi ya kutengeneza barakoa binafsi, vaa barakoa kwa kuzingatia mwongozo uliotolewa na wizara hususan katika maeneo ya msongamano na naelekeza elimu juu ya uvaaji wa barakoa iendelee kutolewa na wataalamu wa afya," alisema.

Aliongeza: "Fanya mazoezi mara kwa mara, kumbuka mazoezi yapo ya aina nyingi na unaweza kuchagua kutegemeana na hali ya afya yako na mazingira yako siku hiyo naagiza mwongozo wa mazoezi utolewe kulingana na afya za watu."

Aliagiza wataalamu wa lishe ngazi zote kuandaa daftari la orodha ya vyakula vya asili vinavyopatikana eneo husika na kutoa elimu ya milo ipi iandaliwe kama kielelezo cha lishe bora.

Vilevile, alimwagiza Mfamasia Mkuu wa Serikali na Mkurugenzi wa Tiba kusimamia mwongozo wa huduma kwa makundi maalum na madirisha ya huduma za afya kwa wazee yaimarishwe sambamba na kliniki za magonjwa sugu.

"Makundi maalumu ya watu wakiwamo wenye umri mkubwa (wazee), watu wenye uzito uliopitiliza (wanene) na watu wenye magonjwa sugu (muda mrefu) mfano pumu, shinikizo la juu la damu, kisukari, magonjwa ya moyo na figo. Kundi hili mara nyingi huathirika zaidi na magonjwa ya kuambukiza kutokana na hali ya kinga zao kuwa haiko imara zaidi," alisema.

Dk. Gwajima aliagiza kuwekwa mazingira mazuri ya kupata huduma za afya kwenye vituo kwa kuruhusu baadhi ya dawa za kutibu magonjwa sugu kupatikana kwenye vituo vya afya na zahanati, ili kuwapunguzia kwenda mara kwa mara kwenye hospitali kubwa za halmashauri au mkoa.

Kuhusu matumizi ya tiba asili, alisema wizara inatekeleza wiki nne za elimu ya tiba asili kwa kurusha vipindi mbalimbali vya redio na televisheni kwa kufikia makabila yote kwa lugha zao.

Aidha, alisisitiza dawa zinazofaa kutumika kwenye magonjwa yanayohusu mfumo wa hewa kuwa ni COVIDOL, NIMRCAF, PLANET++, BINGWA, COVOTANXA, UZIMA HERBAL DROPS, BUPIJI, EUCALYPTUS OIL, LEMONGRASS ESSENTIAL OIL.

Alitaja hatua nyingine ni kuepuka misongamano isiyo ya lazima ikiwamo kwenye vyombo vya usafiri na kuitaka wizara husika isimamie kwa kurejea mwongozo wa afya.

"Wahi kituo cha kutolea huduma za afya mara uonapo dalili za maradhi ili watoa huduma wapate nafasi nzuri zaidi ya kutibu, niwatake maofisa afya wanaotoa huduma mipakani kuendelea kuimarisha udhibiti wa magonjwa katika maeneo ya mipakani kwa mujibu wa miongozo husika," alisema.



Wanafunzi wa Shule ya Sekondari Rundugai, Kijiji cha Chekimaji, Kata ya Masama Rundugai, wilayani Hai, mkoani Kilimanjaro, wakivuka juu ya ukuta wa chanzo cha maji cha skimu ya Mtambo juzi, kutokana na kukosekana kwa kivuko katika eneo hilo, jambo ambalo ni hatari hasa nyakati za masika. **PICHA: MARY MOSHA**

# Muhimbili kutoa huduma ya kujifukiza

**Na Yasmine Protace**

HOSPITALI ya Taifa Muhimbili (MNH), imesema kwa kutambua umuhimu wa tiba asili, itafunga mashine za kujifukiza kwa ajili ya wagonjwa ambao wamekuwa wakihitaji huduma hiyo wanapokuwa wakipatiwa huduma za kibingwa.

Hayo yalibainishwa jana na Mkuu wa Kitengo cha Habari na Uhusianowa Hospitali hiyo, Aminieli Aligaesha, kwamba hospitali itaweka sifa na viwango gani vya mtu kuingia kwenye mashine hiyo kwa kuwa huduma hiyo itakuwa kama nyongeza katika kuwahudumia wananchi wanaofika kupata huduma.

Alisema hayo jijini Dar es Salaam wakati wa ziara ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, ya kuwatembelea wazalishaji wa bidhaa za tiba asili.

Wazalishaji hao ni NIMRCAF, Uzima Herbar Drops, FUKIZA UDANOL, Bingwa Mix spices na Bupil za jijini Dar es Salaam.

Aligaesha alisema hospitali hiyo, imenunua mashine nne ambazo tatu zitafungwa kwenye tawi la Upanga na moja kwenye Mloganzila, na kwamba zinatarajiwa kufungwa mwishoni mwa wiki hii.

Baada ya kuwatembeleza wazalishaji hao, Waziri Gwajima alisema bidhaa zote zinazotengenezwa na wataalamu wa tiba asili lengo lake ni nchi kuwa na njia mbadala kwa njia yoyote.

"Tiba asili ilikuwapo tangu muda mrefu toka miaka ya 1990, na ilishaandikwa kwenye maandiko ya wizara pamoja na Sera ya Afya ya Mwaka 2007, hivyo bidhaa zote zilizotengenezwa na wataalamu wa tiba asili lengo ni kuwa na nia ya kuitafuta tiba kama nchi kwa njia yoyote," alisema.

Dk. Gwajima alisema umefika wakati sasa wa kuzalisha kwa pamoja ili kuitendea haki Ilani ya uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa kuwa na viwanda na kufanya utafiti kwa kuinua bidhaa za tiba asili.

"Lazima tuhitaji mkono wa vyuo vikuu ili kwenda kama timu badala ya kubeba suala la nchi kama la wizara moja, nyinyi UDSM (Chuo Kikuu cha Dar es Salaam) mnashirikiana vipi na China?" Alihoji.

# Zuio la RC matangazo ya misiba lazua jambo

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

BAADA ya kuanza kutekelezwa kwa marufuku ya magari ya matangazo kutangaza misiba barabarani iliyotolewa na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila hivi karibuni, umoja wa wamiliki wa magari ya matangazo na washereheshaji umeibuka na kudai kuwa haukushirikishwa kuhusu hatua hiyo.

Katibu wa Umoja huo, Emmanuel Abel, alisema jana kuwa katazo hilo liliwashtusha na wanakusudia kufanya mkutano kujadiliana namna ya kufanya maridhiano na serikali ili ikiwezekana shughuli hiyo iendelee kufanyika.

Aliwataka wanachama wa umoja huo kuendelea kuwa watulivu na wasiifanye shughuli hiyo wakati wakisubiri majadiliano ambayo yataleta mwafaka.

“Hii kazi ni miongoni mwa ajira ambazo tumeamua kujiajiri. Tumekuwa tukijiingizia kipato na hata halmashauri imekuwa ikiingiza mapato kwa sababu kila tunapotaka kutangaza, tunalipia Sh. 50,000 ili tupewe kibali cha kutangaza,” alisema Abel.

Hezron Mwanditili, mmoja wa wamiliki wa magari hayo ya matangazo, alisema wamekuwa wakiajiri watu wengi kwenye shughuli hizo ikiwamo madereva, watu wa mziki na washereheshaji na hivyo kukataza ni kuua ajira za watu. Alisema shughuli hiyo ni miongoni mwa shughuli za kijamii na hivyo wananchi wamekuwa wakizitegemea kuendesha maisha yao kwa kutumia shughuli hizo.

Alisema hawaelewi sababu hasa ya kukataza matangazo hayo kwa maelezo kuwa baadhi ya wananchi wamekuwa wakiyakodi magari hayo na washereheshaji ili kujifariji baada ya kufiwa na ndugu zao.

“Hatuelewi sababu hasa ya kukataza matangazo haya, yawezekana pengine wanadhani ndiyo yanayosababisha vifo vya watu kwenye jamii au yanawakera kwa sababu gani? Pengine wangetuelewesha, tungeelewa lakini hawakutuhusisha,” Mwanditili alalamika.

Baadhi ya wananchi waliozungumza na Nipashe kuhusu katazo hilo, walibainisha kulifurahia wakidai matangazo hayo yalikuwa kero barabarani kiasi kwamba walikuwa wanayachukia.

Mmoja wa wananchi hao, Emmanuel Mwankapa, mkazi wa Ilolo jijini hapa, alisema kila siku walikuwa wanayasikia matangazo hayo barabarani, akidai yalikuwa yanakwamisha hata shughuli zao kwa kuacha kufanya kazi na kuanza kusikiliza kinachotangazwa.

“Tunamshukuru sana mkuu wa mkoa kwa kukataza matangazo haya. Ilikuwa ukikaa pale Soweto, kila muda ni matangazo hayo mpaka inakuwa kero. Ninaamini sasa hivi kelele zitapungua mjini,” alisifu.

Februari 22, mwaka huu, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Chalamila, alipiga marufuku matangazo hayo huku akiwataka wahusika wayafanyie maeneo ya nyumbani inakokuwa misiba, kanisani na misikitini wanakofanyia ibada na makaburini.Chalamila alitangaza katazo hilo kuanza kutekelezwa jana na kubainisha kuwa alikuwa amesambaza barua kwenye mamlaka mbalimbali kwa ajili ya utekelezaji wa suala hilo.

# Mwekezaji akana kulima bangi

**Na Godfrey Mushi,**

MWEKEZAJI raia wa Poland, Damian Jankowski, ambaye anakabiliwa na kesi ya ulimaji wa dawa za kulevya aina ya bangi na kufanya mauzo ndani na nje ya nchi, amedai kuwa eneo analodaiwa kulima bangi ya kisasa miche 729, alikuwa ameotesha michikichi.

Pia amedai siku ambayo alipelekwa Kituo Kikuu cha Polisi Moshi, polisi walimpa makaratasi atie saini na walipoona haelewi na anasita kutia saini, walimtishia kwa bastola.

Jankowski na wenzake watatu ambao ni mkewe Eliwaza Pyuza, mfanyabiashara Hanif Kanani na Boniface Kessy, wanakabiliwa na mashtaka manne ya kulima bangi, matumizi ya bangi, kufanya mauzo na kusafirisha bangi.

Akiongozwa kutoa ushahidi wake jana na Wakili wa Utetezi Faygrace Sadala, katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Moshi, Jankowski alidai kwamba yeye havuti bangi, isipokuwa kuna uwezekano akawa amepata athari ya dawa hizo kwa kuwa alikaa karibu na moto uliochoma maua yanayodaiwa kuwa ni bangi.

Kesi hiyo namba 79 ya mwaka 2020, inasikilizwa na Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Bernazitha Maziku.

Katika ushahidi wake, Jankowski alidai kuwa baada ya kujenga ukuta kwenye eneo la Nji Panda ya Himo, alilomnunulia mwanawe wa kike, Maryssa, kwa ajili ya kumjengea nyumba, alikuwa ameotesha michikichi.

Aliendelea kudai kuwa maua aliyoyaotesha katika eneo hilo yalikuwa na ukubwa wa robo hekari.

“Sijawahi kuwa na bangi nyumbani, mke wangu (Eliwaza) hajui chochote kuhusu bangi na siku ya Februari 9, 2020, ndiyo mara ya kwanza kuona hayo maua pale Himo.

“Baada ya kufika Himo, Polisi walituambia tung’oe na tuyasambaze hayo maua na baada ya hapo wakaangalia uzito wa hayo maua yakiwa na mizizi yake na udongo na kuyachoma,” alidai.

Alipoulizwa na Wakili wa Serikali, Ignas Mwinuka, wakati wa mahojiano kwamba asali iliyokamatwa nyumbani kwake kama ndiyo ile iliyoonyeshwa mahakamani, shahidi huyo alikiri ndiyo halisi na alikuwa anaitumia na familia yake kwenye chai, badala ya sukari.

Februari 17, mwaka huu, Mahakama hiyo ilimwona Jankowski na wenzake watatu ambao ni raia wa Tanzania, wana kesi ya kujibu katika mashtaka hayo.

Hakimu Maziku aliwaona wana kesi ya kujibu baada ya upande wa mashtaka kufunga ushahidi wa mashahidi wa upande wa mashtaka.

Upande wa mashtaka ukiongozwa na mawakili wa serikali kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka (NPS), Ignas Mwinuka na Verdiana Mlenza, ulifunga ushahidi wake baada ya mashahidi 11 kutoa ushahidi wao pamoja na kuwasilisha vielelezo 36.

Katika hati ya mashtaka, washtakiwa hao wanakabiliwa na mashtaka manne ambayo ni kulima dawa za kulevya kinyume na kifungu cha 11 (1) (a) cha Sheria ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Namba 5 ya Mwaka 2015.

Mshtakiwa wa kwanza, pili na wa tatu wote kwa pamoja wanadaiwa kuwa Februari 8, mwaka jana, huko katika eneo la Njia Panda ya Himo, Wilaya ya Moshi mkoani Kilimanjaro, walikutwa wamelima miche ya bangi 729.

Wakati kosa la pili ambalo linawakabili mshtakiwa wa kwanza, pili na wa tatu, ni kusafirisha bangi kinyume na kifungu cha 15A (1) (2) (C) cha Sheria ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Namba 15 ya Mwaka 2017 kama ilivyofanyiwa marejeo.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI**

**TAASISI YA TEKNOLOJIA YA UJENZI**
**“INSTITUTE OF CONSTRUCTION TECHNOLOGY (ICoT)”**

## TANGAZO LA KOZI YA UKARABATI NA MATENGENEZO YA BARABARA KWA KUTUMIA TEKNOLOJIA STAHIKI YA NGUVU KAZI ‘LBT’

**1. Utangulizi:**
Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi “Institute of Construction Technology (ICoT)” ni Chuo cha Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi chenye makao yake makuu katika Manispaa ya Morogoro. Chuo kinawatangazia wananchi wote kuwa kinatarajia kuendesha kozi ya Ukarabati na Matengenezo ya Barabara za Udongo / Changarawe kwa kutumia Tekinolojia Stahiki ya Nguvukazi katika tawi lake lililopo Mkoani Mbeya, Wilaya ya Rungwe mahali kilipokuwa Chuo cha ATTI-Mbeya kama ifuatavyo:-

| No | JINA LA KOZI | TAREHE YA KUANZA MAFUNZO |
|---|---|---|
| 1 | Kozi ya Ukarabati na Matengenezo ya Barabara za Changarawe kwa Kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi.(Kozi Na.26) | **Wiki Kumi (10)**<br>05/04/2021 - 11/06/2021 |
| 2 | Kozi maalumu ya vikundi vya wanwake na vijana ya juu ya ukarabati na matengenezo ya barabara kwa kutumia teknolojia Stahiki ya Nguvukazi | **Wiki Nne (4)**<br>17/05/2021 - 11/06/2021 |
| 3 | Kozi ya uwekaji wa tabaka la Lami kwenye barabara za miji na vijiji (‘Bituminous surfacing of low traffic volume roads’) kwa Kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi. | **Wiki Nne (4)**<br>**30/08/2021 - 24/09/2021** |

**2. Masomo yatakayofundishwa: -**

(a) Kozi maalumu ya vikundi vya wanawake na vijana: Washiriki watajifunza maada mbali mbali juu ya ukarabati na matengenezo ya barabara za changarawe kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi pamoja na maada shirikishi ambaz o ni utaratibu wa kufungua kampuni kwa vikundi, utaratibu wa kujaza kitabu cha zabuni, uashi(masonry), tekinolojia ya udongo na zege. Kipekee, kozi hii imelenga kumwezesha mshiriki kupata ujuzi wa kufanya na kusimamia kazi za matengenezo ya barabara hasa matengenezo ya kawaida yaani ‘Routine/Reccurent maintenance’.

(b) Kozi ya ukarabati na matengenezo ya Barabara za Udongo / Changarawe: Washiriki watajifunza mambo mbali mbali juu ya ukarabati na matengenezo ya barabara kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi.Pia, watajifunza mambo mbali mbali juu ya: mpango wa kazi (Planning), Uongozi sehemu za kazi na mbinu za usimamiaji wa kazi, vipimo vya kazi, usimamiaji wa mikataba, Uwekaji wa tabaka la changarawe pamoja na ujenzi wa makalavati. Kozi hii imekusudia kumwezesha mshiriki kupata ujuzi wa kutosha katika kufanya na kusimamia kazi za ukarabati na matengenezo ya barabara za changarawe / udongo kwa ubora wa hali ya juu.

**3. Njia za ufundishaji**
Mafunzo yatafanyika KATIKA AWAMU MBILI; awamu ya kwanza itakuwa nadharia (darasani) na awamu ya pili itakuwa ni mafunzo ya vitendo.

**4. Malengo ya kozi**
Masomo katika kozi hizi yamelenga kumpatia mshiriki mbinu mbali mbali juu ya matumizi ya Tekinolojia Stahiki ya Nguvukazi katika:

i. Kufanya na kusimamia kazi za matengenezo ya barabara hasa matengenezo ya kawaida yaani ‘Routine/Reccurent, Periodic and Emergency maintenance’;
ii. Kufanya na kusimamia kazi za ukarabati wa barabara yaani ‘road rehabilitation’;
iii. Kuendesha na kusimamia miradi ya matengenezo na ukarabati wa barabara;
iv. Kwa wajasiriamali, masomo haya yatawawezesha kujiajiri kwa kufungua kampuni za ujenzi wa barabara zinazotumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi yaani “SPECIALIST CIVIL WORKS-LABOUR BASED CONTRACTORING FIRMS” kisha kupata sifa za kisheria za kununua kazi za miradi ya ujenzi au ukarabati wa barabara zinayotolewa na TARURA au TANROADS.

**5. Walengwa wa Mafunzo haya ni:-**

a) Wahandisi wote wa barabara kutoka sekta ya Umma na binafsi,
b) Mafundi Sanifu wa barabara kutoka sekta ya Umma na binafsi,
c) Wasimamizi wa Miundombinu (Estates Managers) toka taasisi mbalimbali za Umma na Binafsi,
d) Makandarasi wenye nia ya kujenga au kuimarisha uwezo wa kazi zao za matengenezo / ukarabati wa barabara kwa kutumia Tekinolojia Stahiki ya Nguvukazi na,
e) Watu binafsi wenye uzoefu katika kazi za barabara au majengo na wanaohitaji kujiendeleza na kujifunza zaidi kazi za barabara.

**6. Lugha ya mafunzo:-**
Lugha itakayo tumika katika kozi ya Ukarabati na Matengenezo ya Barabara za Changarawe kwa Kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi ambayo itaendeshwa kwa muda wa wiki kumi (10) ni kiingereza wakati kozi maalumu ya vikundi vya wanawake na vijana itaendeshwa kwa kutumia mchanganyiko wa lugha ya kiingereza na kiswahili.

**7. Gharama za Mafunzo:-**
**Gharama za mafunzo zitakuwa kama ifuatavyo:**

| JINA LA KOZI | MUDA (Wiki) | ADA (TSH.) |
|---|---|---|
| Kozi ya Ukarabati na Matengenezo ya Barabara za Changarawe kwa Kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi. | Kumi (10) | 1,600,000/= |
| Kozi maalumu ya vikundi vya wanwake na vijana ya juu ya ukarabati na matengenezo ya barabara kwa kutumia teknolojia Stahiki ya Nguvukazi | Nne(4) | 500,000/= |
| Kozi ya uwekaji wa tabaka la Lami kwenye barabara za miji na vijiji (‘Bituminous surfacing of low traffic volume roads’) kwa Kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi. | Nne(4) | 1,000,000/= |

Ada ya ushiriki zilipwe kwa kutumia ‘control number’ itakayotolewa kwa mtu yeyote atakayehitaji mafunzo kwa kuwasiliana na uon gozi mapema kabla ya kozi kuanza. Inashauriwa kuwa ada ilipwe angalau wiki mbili kabla ya kozi kuanza.

**8. Namna ya Kutuma Maombi ya Kozi hizi:-**
Wale wote watakao hitaji kujiunga na kozi yoyote kati ya hizi zilizotajwa wanatakiwa kutuma maombi yao Chuoni ICoT, tawi la Mbeya au Morogoro kwa kutumia anuani ya Posta au barua pepe zilizotolewa hapa chini au wanaweza kupiga simu kwa maelezo zaidi.

**Kumbuka:** Kuna nafasi za malazi ishirini (20) tu kwa kila kozi; hivyo, inashauriwa kutuma maombi mapema iwezekanavyo.

**Wasiliana nasi:**

**Mkuu wa Chuo - ICoT**
**ICoT – Mbeya / Sogea, Wilaya ya Rungwe (Tukuyu)**
**S.L.P 1957, MBEYA,**

**Simu: 025 295 7484/5; 0787 059 555; 0769 317 404; 0765 251 509**
**Nukushi: 025 295 7486**
**Barua pepe: attimbeya@mow.go.tz, attimbeyafrica@gmail.com**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Usajili wa Vicoba usimamiwe vizuri

**JUZI** Benki Kuu ya Tanzania (BoT), ilifafanua na kutoa msimamo wa tozo na kodi ambazo zinasemekana kuwa zitatozwa kwenye vikundi vidogo vidogo yaani Vicoba.

Ufafanuzi huo umetolewa ukiwa umebaki mwezi mmoja na siku nne kufika tarehe ya mwisho ya usajili wa taasisi zinazotoa huduma ndogo za fedha, taasisi zinazotoa mikopo bila kupokea amana za umma ikijumuisha kampuni za kukopesha, kutoa huduma ndogo kwa njia za kidijitali na watu binafsi wanaokopesha.

Wengine ni vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo (SACCOS) na Vicoba. Aidha, sheria imebainisha kuwa benki zinazofaya biashara ya huduma ndogo za benki na huduma ndogo za fedha zitasimamiwa kwa mujibu wa sheria ya benki na taasisi za fedha ya mwaka 2006.

Jukumu la kisheria la BoT ni kusimamia na kufuatilia, kutunga kanuni na kusimamia watoa huduma, lakini sheria imetoa mwanya wa kukasimisha mamlaka na majukumu yake ya kutoa tangazo kwenye Gazeti la Serikali.

SACCOS zinasimamiwa na Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC) na VICOBA ni mamlaka za serikali za mitaa ambazo ni halmashauri na manispaa.

Aidha, BoT ilieleza imesikia malalamiko ya wananchi kutozwa fedha kwa ajili ya usajili ambao bado haujaanza kwa kuwa ilisubiri mwongozo, kukamilika kwa mfumo wa usajili na elimu kwa maofisa maendeleo ya jamii.

Tayari mifumo imekamilika na mafunzo kwa maofisa maendeleo ya jamii, ambao sasa wanawajibika kutangaza kuanza usajili kwenye maeneo yao na ndani ya siku 14 vikundi viwe vimepata usajili.

Mwongozo uko bayana na kanuni zimefafanua kila kitu ni wajibu wa maofisa maendeleo ya jamii kufikisha elimu kwa umma ili kuondoa mkanganyiko uliokuwapo kuwa kuna kodi zitakazotozwa kwenye fedha za wanakikundi kwa mwezi na mwisho wa mwaka faida nayo itatozwa kodi.

Hali hiyo imesababisha baadhi ya vikundi kuanza kuweka fedha nyumbani na kuachana na utaratibu rasmi wa kwenda benki, huku wengine wakivunja vikundi kwa madai kuwa fedha zao zitatozwa kodi kubwa.

Baadhi ya vikundi vilijikuta chini ya baadhi ya SACCOS na wadhamini ili kukimbizana na usajili, ambako huko walitozwa fedha za usajili, jambo ambalo BoT imelipinga na kutaka watu kupata taarifa sahihi kutoka sehemu sahihi.

Ni matumani yetu kuwa baada ya maofisa maendeleo ya jamii kuelimishwa watafikisha elimu kwa wananchi na vikundi vinavyofika kwenye ofisi zao kwa ajili ya usajili, kwa kuwa kumekuwa na vikwazo vingi katika kusajili.


Kama ambavyo BoT inasisitiza kuwa hakuna tozo zozote zinazofanywa na mamlaka yoyote katika usajili, tunatarajia halmashauri zitasimamia kwa ufasaha kuhakikisha kuwa vikundi havikatishwi tamaa kwa sababu ambazo hazipo au kutozwa fedha ambazo kimsingi hazistahili.

Ni matarajio yetu kuwa TAMISEMI na madiwani watafuatilia kwa kina suala hili, ili kuondoa usumbufu ambao vikundi vinaupata na mwisho kujiendesha kwa siri au kuvunja vikundi ambavyo viliwakwamua wengi kimaendeleo.


Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com


## Muungwana Lazima Nilonge



# Kusubiri tamko kuu ni kuchelewa kuchukua tahadhari maradhi haya

Na Sabato Kasika

**KATIKA** siku za karibuni kumekuwapo mjadala kwenye mitandao ya kijamii, baadhi ya watu wakitaka serikali itoe tamko kuhusu tatizo la upumuaji, huku wengine wakitaka jamii ichukue tahadhari badala ya kusubiri tamko.

Wote kama Watanzania wana haki kutoa maoni, lakini maoni yasichangie kupotosha jamii, badala yake yaisaidie kuchukua hatua zinazoshauriwa na wataalamu wa afya ili kukabiliana na tatizo hilo.

Binafsi, ninaamini Watanzania wengi wanajua kila kitu kuhusu ugonjwa huo tangu dalili zake hadi njia za kujikinga. Kama mtu unajua tatizo na njia zake za kujikinga, kuna haja gani ya kusubiri tamko?

Watu kukaa na kuendelea kuhoji au kuitaka serikali itamke kuhusu kuwapo kwa ugonjwa huo nchini ni matumizi mabaya ya muda, ambao ungetumika kufanya mambo mengine ya muhimu. Kwanini mtu asichukue hatua zinazotakiwa kama anaona kuna tatizo mbele yake na kubaki akisubiri tamko? Tamko litasaidia nini zaidi ya kuzingatia masharti ya kuepuka ugonjwa huo? Hata kama hakuna tamko la serikali, kila Mtanzania anatakiwa kufanya sehemu yake kwa kuchukua tahadhari za kiafya ili kujikinga na maambukizo, kwa kuzingatia kwamba, Tanzania siyo kisiwa.

Watu kuendelea kuhoji na kutaka tamko, ni sawa na kuchelewa kuchukua hatua zinazoelekezwa na wataalamu wa afya na mwisho wake ni matatizo ya kujitakia. Tayari serikali imeshasema haijamzuia mtu yeyote kuvaa barakoa na taratibu nyingine zinazoshauriwa na wataalam wa afya, lakini ikashauri kutumia barakoa zilizotengenezwa nchini. Kukaa na kuendelea kusubiri tamko ni kupoteza muda. Badala yake, kila mmoja anapaswa kutumia tamko kuchukua tahadhari dhidi ya ugonjwa huo, kama ambavyo wataalamu wa afya wanaelekeza kwa ajili ya kukabiliana nao. Ni vyema kila mkazi nchini afanye sehemu yake, kwa kuzingatia maelekezo ya watu wa afya, ambayo kimsingi yameshawekwa wazi na kuendelea kuhoji au kutaka tamko bila kujikinga ni sawa na kujitafutia matatizo. Mwaka jana, Tanzania ilipitia tatizo hilo na kulazimika kufungwa baadhi ya huduma kama shule, huku watu wakitakiwa kufuata maelekezo ya wataalamu wa afya, ikiwamo kunawa kwa maji tiririka, vitakasa mikono, kuvaa barakoa na kuepuka mikusanyiko.

Vilevile, hatua nyingine zinazotakiwa kuchukuliwa ni pamoja na kufunika mdomo na pua pale mtu anapopiga chafya na kukohoa, lengo ni kusaidia kujikinga au ueneaji maradhi hayo au ya namna hiyo yanayoendelea kuisumbua dunia.

Aidha, kuna tiba na kinga mbadala wa kukabiliana na ugonjwa huo, ni upigaji nyungu kujihakikishia usalama kiafya ingawa bado baadhi ya watu wanaendelea kuhoji kitu ambacho wanakijua. Tahadhari hizo zilienda sambamba na kuagiza madereva wa daladala kutojaza abiria kupita kiasi na badala yake wakawa ni wale waliokaa kwenye viti tu. Lakini ni ajabu kushuhudia, kuna wanahoji mambo ambayo wanayajua.

Hayo yote ni wazi kwamba yanajulikana, lakini cha ajabu ni watu kuanza kuhoji na kutaka tamko ili kujikinga na tatizo la kupumua kana kwamba hawajui lolote kuhusu mbinu za kukabiliana na ugonjwa huo au maradhi yanayoenea kwa namna hiyo. Inawezekanaje mtu ukaona tatizo mbele yake, badala ya kuchukua hatua za kulikwepa au kukabiliana nalo. Anasubiri kwanza hadi asikie tamko. Sidhani kama itakuwa sahihi kufanya hivyo.

kunapaswa tamko lisiwe kikwazo cha kushindwa kuchukua tahadhari, badala yake jamii yenyewe ihamasishane, ili kila mtu azingatie kwa vitendo maelekezo yanayotolewa na wataalamu wa afya.

Wakati hayo yakifanyika, madereva na makondakta wa daladala zinazotawala hasa mijini nao wasisubiri tamko ndipo waache mtindo wa kujaza abiria kupita kiasi katika magari yao.

Ikumbukwe kuwa kwenye tatizo la upumuaji, watu wanatakiwa kupeana nafasi katika kukaa, ili kuepuka kuambukizana, hivyo hata kwenye usafiri ni muhimu hali hiyo irudi kama ilivyokuwa mwaka jana.

Kwa Jiji la Dar es, siyo vibaya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), ikaruhusu magari binafsi yakaingia katika ya jiji kusaidiana na daladala kubeba abiria, ili kupunguza msongamano ndani ya daladala.

Mwaka jana LATRA ilichukua hatua kama hizo, kama inawezekana, ichukue tena kama sehemu ya kuzingatia kile ambacho kinashauriwa na wataalamu wa afya kwa ajili ya kujikinga na maradhi hayo.

HABARI KITAIFA

# Nzige wadhibitiwa kwa 70% Longido

**Na Asraji Mvungi,** LONGIDO

WATAALAMU wanaosimamia zoezi la kuangamiza nzige katika Wilaya ya Longido mkoani Arusha, wametoa matokeo ya awali yanayoonyesha kuwapo kwa mafanikio kwa asilimia 70.

Wataalamu hao akiwamo Oshingi Shilla, kutoka TPRI amesema hadi sasa nzige waliokuwa wamevamia eneo la hekta 425 katika wilaya hiyo, hawajaonekana tena, na kwamba wanahofiwa kuwa wameangamia na kazi ya kuwafuatilia inaendelea.

Akitoa taarifa ya matokeo ya zoezi hilo kwa Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Iddy kimanta, aliyetembelea eneo lililokuwa limevamiwa, Shilla alisema kwa kawaida wadudu hao wanapopigwa dawa inawachukua wastani wa saa 24 hadi 72 kuangamia.

Hata hivyo, licha ya Mkuu wa Mkoa kutembelea eneo lililopigwa dawa kwa lengo la kujionea mabaki ya nzige waliokufa, mtaalamu huyo alimwambia kuwa kutoonekana kwa mabaki hayo sio tatizo kwani dawa waliyopiga inaendelea kufanyakazi na matokeo yataendelea kuonekana.

"Mheshimiwa mkuu wa mkoa huwa sio rahisi wadudu hawa kufa kwa mara moja, lakini wataendelea kufa kadiri siku zinavyokwenda alisema Shilla.

Kwa upande wake Mbunge wa Longido, Dk. Steven Kiruswa, alisema licha ya mafanikio hayo wanaendelea kuimarisha mtandao wa kupata taarifa za mwenendo wa nzige hao kwa kuwatumia wananchi, wakiwamo vijana wa jamii ya wafugaji.

Kwanza nawashukuru sana wananchi wa Longido kwa kutoa ushirikiano mkubwa wa kudhibiti nzige hawa haswa kwa kutoa taarifa na tunawaomba mwendeleze utaratibu huo, na pia kwa kuendelea kuheshimu maekekezo yakiwamo ya kutopeleka mifugo kwenye maeneo yaliyopigwa dawa," alisema Dk. Kiruswa.

Akizungumza baada ya kutembelea eneo lililopigwa dawa ya kuangamiza nzige, RC Kimanta alisema nzige waliokuwa wanatishia amani wamedhibitiwa, na pia hawajaleta madhara makubwa.

Kwa mujibu wa Kimanta, licha ya athari ya kufungwa kwa shule tatu za msingi kwa muda wa siku nne, hakuna madhara mengine yaliyotokana na wadudu hao, na aliwapongeza wananchi wa Longido kwa kuwa wepesi wa kutoa taarifa sahihi na kwa wakati za nzige hao na kwenye mamlaka zinazohusika.

"Mafanikio haya yanayoonekana, yakiwamo ya kudhibitiwa kwa nzige hawa kabla hawajaleta madhara...ni matokeo ya taarifa sahihi zilizotolewa na wananchi, na mmefanya jambo ambalo ni mfano wa kuigwa," alisema Kimanta.

Baadhi ya wananchi walipongeza hatua zilizochukuliwa na serikali kudhibiti wadudu hao ambao walikuwa wanatishia usalama wa mifugo yao.



Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe (aliyevaa kofia), akiwa na viongozi wa Wilaya ya Longido, mkoani Arusha juzi, kukagua eneo la kijiji cha Kimokouwa, baada ya ndege maalum kunyunyiza kiuatilifu (sumu) ya kuua makundi ya nzige waliovamia kwenye mashamba ya wakulima wa eneo hilo. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# BoT yapiga marufuku uuzaji noti chakavu

**Na Salome Kitomari,** MTWARA

BENKI Kuu (BoT) imepiga marufuku biashara ya kuuza fedha chakavu, ikizitaka benki na taasisi za fedha kutoa fedha safi na kurudisha kwao zilizo chafu ili ziondoke kwenye mzunguko. Meneja wa benki hiyo anayeshughulikia noti na sarafu, Ilulu Ilulu, alitoa agizo hilo jana wakati wa semina kwa waandishi wa habari za uchumi na biashara inayoendelea mjini Mtwara.

Alisema katika maeneo ya masoko na minada kumekuwa na watu ambao wananunua fedha chakavu kwa bei pungufu na kwenda kubadilisha BoT kwa bei kamilifu kwa kuwa kwa mujibu wa sheria, fedha inabadilishwa kwa fedha kamili.

"Hairuhusiwi kuuza fedha chafu, tunataka wananchi kutoa taarifa, fedha inabadilishwa kwa fedha. Tuna sera ya kuhakikisha tunatoa noti na sarafu chafu kwenye mzunguko na kuhakikisha safi zinapatikana.

"Taasisi za fedha zinajua, zinapaswa kuja BoT kuchukua noti safi na kurudisha chafu ambazo tuna jukumu la kuziharibu kisheria," alifafanua.

Alisema wanachofanya wauzaji, wanazikusanya kwa bei pungufu, akitolea mfano noti ya Sh. 10,000 wanazinunua kwa Sh. 9,000, hivyo wakizifikisha BoT, wanapata faida ya Sh. 1,000 kwa kila noti.

# Dar kinara ukatili wa wanawake

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, ametaja mikoa mitano yenye kiwango cha juu cha ukatili wa wanawake kwa mwaka 2019/20, huku Mkoa wa Dar es Salaam ukiongoza.

Katika Mkoa wa Dar es Salaam matukio yaliyoripotiwa ni 2,618, ukifuatiwa na Arusha (1,393), Tanga (1,352), Lindi (1,161) na Manyara (968).

Kufuatia hali hiyo, ameagiza wataalamu wa maendeleo ya jamii kusaidia mikoa hiyo kubaini tatizo la kuongoza kwa vitendo hivyo licha ya kuwa na maendeleo makubwa.

Dk. Gwajima aliyasema hayo, jana, alipokuwa akifungua Kongamano la Chama cha Wataalamu wa Maendeleo ya Jamii Tanzania (CODEPATA), jijini hapa.

"Eti mikoa iliyoongoza ushangae wewe wanasema maendeleo ni makubwa wanaendeleza na matukio ya ukatili...Tatizo nini kwenye hii miji yetu mikubwa yenye TV kila nyumba, wasomi na barabara zipo mjini, twendeni tukawasaidie tatizo ni nini?" Alihoji.

Alisema takwimu hizo sio nzuri na haipendezi na inahitaji kuimarisha nguvu kubwa ya kuzungumza na jamii kwa kutumia taaluma yao.

"Tunataka katika miaka ijayo hii hali ishuke, serikali itaendelea kuchukua hatua za kukabiliana na ukatili, hizi kamati za MTAKUWWA hakikisheni zinasimamia na kutokomeza ukatili wa wanawake na watoto kwenye maeneo yao," alisema.


MABUNDA AUCTIONEER MART CO. LTD
P.O. Box 61424 DAR ES SALAAM, TANZANIA
TELL: 0787129539/0719656930
Dealers in: Auctioneer & Debt collection
Email: mabundacompanyltd@gmail.com

TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kwa idhini tuliyopewa na BUBALE LIMITED tutauza kwa mnada wa hadhara vifaa **vilivyopo Kilosa Morogoro** kuanzia tarehe 10/03/2021 na kuendelea baada ya kutoka kwa tangazo.

1. Harvest Class CS228
2. Tractor Massey Fergusson 9240
3. Tractor Massey Fergusson 9240 - as it is stands
4. Trailer 18 t
5. Crops sprayer Nodet
6. Planter Kinze 3650 – 16/31
7. Fertilizer sprayer 24m Amazon
8. Ripper / per ripper
9. Crusher
10. Bulldozer Caterpillar D5 LPG
11. Bulldozer Caterpillar D5 LPG - as it is stands
12. Excavator 10 t Case

MASHARTI YA MNADA
1. Dhamana itauzwa kama ilivyo
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa siku ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14) Kushindwa kufanya hivyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25% na mnada kurudiwa.
4. Taratibu za kuona au kukagua vifaa, zitafanyika tarehe 01/03/2021 kabla ya kufanyika kwa mnada

Kwa mawasiliano zaidi
0787129 539/0655 129 539
Email: mabundacompanyltd@gmail.com

HABARI KITAIFA

# Wachimbaji walia ukosefu mawasiliano

**Na Shaban Njia, MBOGWE**

ZAIDI ya wachimbaji wadogo 2,500 wa dhahabu, Rashi ya Nyakafulu, Mbogwe, mkoani Geita, wameiomba serikali kuwajengea mnara wa mawasiliano katika eneo hilo ili kuwasaidia kuwasiliana na wateja wao kwa urahisi.

Walwa Katemi, Mwenyekiti wa Mgodi wa Isanja, aliyabainisha hayo jana wakati akizungumza na vyombo vya habari zilivyofika mgodini hapo kutambua wanavyoshiriki shughuli za maendeleo hasa kwa wananchi wanaozunguka mgodi.

Alisema eneo hilo lina changamoto ya mawasiliano ya simu licha ya kuchangia pato la taifa kupitia sekta ya madini. Jambo hilo, alisema limekuwa likisababisha kuuza madini kwa bei ya hasara bila kutambua kama bei imeshuka au la katika soko la dunia.

"Sisi ni wachimbaji ambao hatutambui bei za madini zinazobadilika kila siku duniani. Tunakwenda kuuza madini kwenye masoko yetu hatutambui kama yamepanda au yameshuka na ili kuondoa wasiwasi huu ni vema tukapatiwa mnara wa mawasiliano wa simu," alisema Katemi.

Naye Pius Karau, mmoja wa wachimbaji, alisema eneo hilo linaongoza kwa kuwa na madini mengi mkoa mzima wa Geita, lakini wachimbaji wake hawatambui bei ya soko la dhahabu liko vipi.

Alisema kutokana na kukosekana kwa mawasiliano, wanatambua zaidi hali ya soko wanapokwenda kwenye masoko wakati wa kuuza, hiyo imekuwa ikisababisha wachimbaji kuibiwa wakati wa mauzo.

Pia Karau alisema uwapo wa mawasiliano utasaidia pia kutoa taarifa katika vyombo vya sheria endapo itatokea hali ya viashiria vya uvunjifu wa amani kwa sababu katika maeneo ya migodi kumekuwa kukitokea ajali nyingi ikiwamo wachimbaji kufukiwa na vifusi.

Katika hatua nyingine, Katemi ameiomba serikali kupitia Wizara ya Madini, kuwapatia leseni ya uchimbaji ili kufanikisha kuchangia kikamilifu mapato ya serikali, halmashauri na kuendelea kuchangia masuala ya maendeleo kwa wananchi wanaowazunguka.

Alisema wako wachimbaji wanaotaka kuwekeza katika eneo hilo, lakini wanaogopa mitaji yao kufa kwa kuhofia kutimuliwa na serikali baadaye na kwamba endapo wizara itatoa leseni, wawekezaji wengi watajitokeza na kuajiri vijana wengi ambao wako mitaani hawana shughuli za kufanya.

# Mradi wa usajili ardhi vijiji waanza

**Na Munir Shemweta,** MBEYA

OFISI ya Ardhi Mkoa wa Mbeya kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, imeanza kutekeleza mradi wa usajili ardhi vijijini katika vijiji 20 kama mradi wa mfano unaotarajiwa kutekelezwa katika halmashauri zote za mkoa.

Mradi huo unatekelezwa kwa kutumia mfumo wa kisasa wa upimaji na uchukuaji picha za anga na wanufaika wake wanachangia gharama za kupanga, kupima na kumilikishwa vipande vyao kwa kuzingatia dhana ya 'fit for purpose'. Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Mbeya, Siyabumi Mwaipopo, alithibitisha hayo, juzi, alipowasilisha taarifa ya sekta ya ardhi katika mkoa wake katika kikao baina ya Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula na watendaji wa sekta ya ardhi pamoja na wakurugenzi wa halmashauri za mkoa wa Mbeya.

"Uchangiaji gharama za kupanga, kupima na kumilikishwa ardhi katika mradi huu una mambo mawili ya msingi ambayo ni kuondoa dhana ya utegemezi katika utoaji huduma za ardhi na kufanya umilikishaji ardhi kuwa endelevu," alisema Mwaipopo.

Kwa mujibu wa Mwaipopo, katika kutekeleza mradi huo, wananchi wanaomiliki ekari moja mpaka 10, watachangia Sh. 30,000 na wale wenye mashamba ya ukubwa wa ekari 11 mpaka 50 watachangia Sh. 60,000 huku wenye ekari kuanzia 51 na kuendelea wakichangia Sh. 120,000.

Alisema kupitia mradi huo, vijiji 10 kati ya 20 vitapimwa mipaka na ramani kusajiliwa. Vijiji 13 vitaandaliwa mipango ya matumizi ya ardhi, vinne ambavyo mipango ya matumizi bora ya ardhi inakaribia kuisha muda wake mipango yake itarejewa upya na vyeti vya ardhi vya vijiji 10 vitaandaliwa katika eneo la mradi na kila kipande cha ardhi kitapimwa na kupatiwa hati miliki ya kimila.

Mwaipopo aliongeza kuwa katika utekelezaji mradi huo, taasisi zote za kisheria zinazohusika na migogoro ya ardhi zitajengewa uwezo kwa kupatiwa mafunzo bora ya uendeshaji mabaraza ya ardhi ya vijiji na kata zote zilizo eneo la mradi.

Pia alisema mabaraza ya ardhi ya vijiji vinane yataanzishwa katika eneo la mradi sambamba na Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Mbarali kuanza kufanya kazi mapema.

Naibu Waziri Mabula aliwataka watendaji wa sekta ya ardhi katika halmashauri za wilaya za mkoa wa Mbeya kuanza kutoa elimu ya kupanga maeneo katika vijiji ili kuepuka ujenzi holela.

"Tuanze kutoa elimu kwa watendaji walioko vijijini, wajue ABC za kupanga maeneo yao kabla hayajaanza kutangazwa maeneo ya upangaji na tukifanya hivyo miji yetu itakaa vizuri na tutaondokana na zoezi la urasimishaji ambalo linamalizika 2023," alisema Dk. Mabula.

Katika hatua nyingine, Mabula aliagiza kufuatiliwa kwa wamiliki wote wa viwanja wenye tozo ya adhabu ya maendelezo yaliyokiuka sheria ya mipango miji katika mkoa wa Mbeya, ili waweze kulipa kiasi wanachodaiwa kama walivyopelekewa ilani za madai.

Kwa mujibu wa taarifa ya sekta ya ardhi, mkoa wa Mbeya una viwanja 154 ambavyo wamiliki wake wamefanya maendelezo kwa kukiuka masharti ya uendelezaji na viwanja hivyo vinadaiwa Sh. 1,074, 830,060 huku Sh. 65,100,000.00 pekee ndizo zilizolipwa.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
SHIRIKA LA UWAKALA WA MELI TANZANIA
TASAC



Pumzika kwa Amani

Mhe. Maalim Seif Sharif Hamad

Makamu wa kwanza wa Rais Zanzibar

1943 - 2021

Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Wafanyakazi wa **Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC)** tumepokea kwa masikitiko makubwa taarifa ya msiba wa **Mhe. Maalim Seif Sharif Hamad**, Makamu wa kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Tunatoa salamu za pole kwa Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, **Mhe. Dkt Hussein Ali Mwinyi**. Familia, ndugu, marafiki na Watanzania wote.

*Mwenyezi Mungu aiweke roho ya Marehemu mahala pema Peponi. AMINA*



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
SHIRIKA LA UWAKALA WA MELI TANZANIA
TASAC



Pumzika kwa Amani

Balozi John William Kijazi

Katibu Mkuu Kiongozi

1956 - 2021

Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Wafanyakazi wa **Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC)** tumepokea kwa masikitiko makubwa taarifa ya msiba wa **Balozi John William Kijazi**, Katibu Mkuu Kiongozi

Tunatoa salamu za pole kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, **Mhe. Dkt John Pombe Magufuli**. Familia, ndugu, marafiki na Watanzania wote.

*Mwenyezi Mungu aiweke roho ya Marehemu mahala pema Peponi. AMINA*

HABARI KITAIFA

# Wataka kunusuru Bonde la Kilombero

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

SERIKALI imetakiwa kuchukua hatua za haraka kudhibiti uharibifu unaofanywa katika Bonde la ardhi oevu la Kilombero, , na vyanzo vingine vya maji katika wilaya za Mvomero na Kilosa katika Mkoa wa Morogoro, kutokana shughuli za kibinadamu

Shughuli hizo ni mifugo,uchimbaji wa madini, kilimo huku vikihatarisha kukosekana huduma ya maji katika mikoa ya Morogoro, Pwani na Dar es Salaam.

Tahadhali hiyo ilitolewa na muikolojia, Asukile Kajuni, kutoka Shirika la GEO Network Limited lilopewa kazi ya kutengeneza mpango mkakati wa uhifadhi na ulinzi wa vyanzo vya maji katika mabonde tisa wakati akiwasilisha mpango huo katika warsha wa wadau ya maji iliyofanyika mjini Morogoro.

Kajuni alisema katika shughuli yao ya kutengeneza mpango huo katika bonde la maji la Wami Ruvu, wameshuhudia wimbi la mifugo, shughuli za kilimo na uchimbaji wa madini ukiharibu kingo za mito na kusababisha kuingiwa kwa matope kwenye vyanzo vya maji na pamoja na kwenye mito ambayo inatiririsha maji kwenye mito mikubwa na kusababisha upungufu wa maji.

Maeneo yaliyokithiri ni Bonde la ardhi oevu la Kilombero, ambalo limevamiwa na idadi kubwa ya mifugo kutoka maeneo mbalimbali na imekuwa ikiharibu vyanzo vingi vya maji hasa katika Kijiji cha Mofu eneo la Kibasila ambapo mifugo hiyo imefikia hatua ya kuhatarisha vyanzo vya maji vinavyoingia katika mto Kilombero. " Kama Mkuu wa wilaya na serikali yake wasipochukua hatua za haraka kudhibiti mifugo iliyopo katika bonde la Kilombero hasa katika kijiji cha Mofu eneo la Kibasila, kuna hatari ya kupungua kwa maji katika mto Kilombero kwani uharibifu wa mifugo ni mkubwa mno... kuna ng'ombe wengi sana wanaharibu vyanzo vya maji," alisema.

Alitaja eneo lingine ni Mgeta ilipo Wilaya ya Mvomero ambapo shughuli kubwa za kilimo zimekuwa zikifanywa katika maeneo ya milima bila kutumia makinga maji, hivyo kuharibu vyanzo hivyo ambavyo vinatiririsha katika mto Morogoro na kuelekea katika mto Ruvu ambao ndio chanzo kikuu cha watumiaji wa maji katika mikoa ya Pwani na Dar es Salaam.

Mwenyekiti wa Bodi ya Maji Bonde la Wami Ruvu, Hamza Sadiki, alisema Wizara ya Maji kupitia bodi za maji za mabonde imepewa jukumu la utunzaji wa vyanzo vya maji, hivyo wameamua kuanza kufanya tathmini ya kuangalia uhalibifu kwenye vyanzo hivyo ili kuja na mpango mkakati wa kuvitunza na kuviendeleza kwa manufaa ya sasa na vizazi vijavyo.

Alisema kupitia mpango huo wameainisha mahitaji ya wadau mbalimbali wa Sekta ya maji kwa kuzingatia wakati uliopo na wakati ujao na umependekeza kazi mbalimbali ambazo zikitekelezwa, zitaweza upatikanaji endelevu wa maji kutoka kwenye vyanzo vya maji.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa, Asajile Mwambambale, alipongeza bonde hilo kuja na mpango huo kwa kushirikisha wadau mbalimbali kwa kuwa utaweza kusaidia matumizi sahihi ya rasilimali hizo za maji hasa katika maeneo ya uchimbaji madini, kilimo na mifugo katika wilaya hiyo.

## SBL yazindua bia mpya mikoa mitatu

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya bia ya Serengeti (SBL), imezindua bia mpya aina ya Guinness Smooth katika mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Manyara na Tanga.

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo jijini Arusha, Meneja Uvumbuzi wa SBL, Bertha Vedastus, alisema: "Bia hii mpya kwenye familia ya Guinness ina ladha ya kipekee ambayo inamfanya kila mnywaji afurahie kila mara anapoitumia na wakati akiwa na marafiki."

Bertha aliongeza: "Bia hii ina hadhi ya kimataifa na imetengenezwa katika kiwanda chetu cha moshi, huku ikitumia malighafi za Kitanzania ikiwamo shayiri inayolimwa katika mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na mingineyo."

"Guinness ina historia ndefu na kongwe ya kutengeneza bia, bidhaa ambazo zimefanikiwa kuteka soko la dunia na kuendelea kuwa kinara," alisema.



Meneja uvumbuzi wa Kampuni ya Bia ya Sarengeti, Bertha Vedastus (wa pili kushoto), akipongezana na wateja wa kampuni hiyo, baada ya uzinduzi rasmi wa bia mpya ya Guinness Smooth, jijini Arusha juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Halmashauri zaelekezwa mazao ya nyuki

**Na Elizabeth Zaya**

MAKAMU wa Rais, Samia Suluhu Hassan, ameagiza kuboreshwa kwa sekta ya misitu na mazao ya nyuki na kuhakikisha kila halmashauri inakuwa na kiwanda cha kuchakata mazao hayo ya nyuki na kuviboresha zaidi vile vya uzalishaji wa mazao ya mbao.

Amesema lengo ni kuongeza mnyororo wa thamani katika mazao ya misitu na nyuki nchini.

"Viwanda vya kuchakata mazao ya nyuki kwa sasa vipo 21, lakini wizara imeongeza viwanda vitatu kwa hiyo tutakuwa na viwanda 26 ambavyo bado havitoshi, katika hali ya kawaida hivi viwanda vidogo tunatakiwa tuwe navyo 200," alisema Samia.

"Tuna halmashauri 186, kwa hiyo kila halmashauri ikiwa na kiwanda kimoja ambacho nacho hakitoshi lakini itakuwa angalau."

Samia alitoa maagizo hayo katika hotuba yake iliyosomwa na Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro, wakati wa uzinduzi wa kongamano la kimataifa la sayansi juu ya mnyororo wa thamani wa mazao ya misitu na nyuki kwa ajili ya maisha endelevu na uchumi wa viwanda.

Alisema kuwa kuna haja ya kuwa na mkakati mahsusi wa kuainisha masoko na tabia zake katika kufanikisha sekta hiyo na kutaka utafiti unaofanyika uwafikie wadau na uandikwe kwa lugha nyepesi.

"Tanzania ina wasomi wengi sana na wanafanya utafiti, katika mazao ya nyuki na misitu, hakuna taasisi nzuri za utafiti Afrika na Kusini mwa Jangwa la Sahara kama za Tanzania, lakini tafiti nyingi zinawekwa kwenye makabati, ni wakati sasa tafiti zifike kwa wadau katika jamii zetu, na kuziandika katika lugha nyepesi," alisema Samia.

Alisema bado nchi haijatumia vizurirasliimali hizo za misitu na nyuki na kwamba kuna haja kuliangalia hilo.

"Uwezo wa nchi wa kuzalisha asali ni tani 134,000, lakini kwa sasa tunazalisha tani 34,000 tu, tunataka mtuambie nini kifanyike ili twende mbali zaidi," alisema.

Samia aliagiza kila halmashauri nchini kuhakikisha inapanda miti milioni 1.5 kila mwaka.

Pia, aligiza kuongeza jitihada katika kusimamia uhifadhi na utunzaji wa mazingira hususani ukataji wa miti.

"Endapo miti yote itakatwa halafu oksijeni itengenezwe kwenye maabara ambayo thamani yake ni Sh. 22.7 kwa mwaka mzima, ni watanzania wangapi wanaweza hilo, watu tutakufa, ndio maana nawaagiza msikate miti kwa sababu hatuna fedha ya kununua hiyo oksijeni ya maabara," alisema Samia.

Aliagiza kuthibiti mifugo na shughuli za kilimo kwenye hifadhi za misitu na kulitaka Jeshi Usu kuhakikisha linathibiti hilo.

Naibu Waziri wa Masiali na Utalii, Mary Masanja, alisema sekta ya ufugaji ya nyuki imeonyesha kuwa inaweza kuchangia sehemu kubwa katika ukuaji wa uchumi.

Alisema wizara imechukua hatua ya kuboresha uzalishaji, uchakataji biashara za mazao ya nyuki ili kuhakikisha inaongeza zaidi pato la taifa.

HABARI KITAIFA

# Serikali yataka umakini wa matumizi dawa za kujifukiza

**Na Elizabeth Faustine,** MWANZA

SERIKALI imewataka wananchi kuwa makini na mchanganyiko wa viungo vinavyotumika kutengeneza dawa ya kujikinga na ugonjwa wa corona.

Lengo ni kuepuka madhara yatokanayo na mchanganyiko huo.

Angalizo hilo lilitolewa na Mkurugenzi wa Tiba na Lishe wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Leornad Subi, wakati akizungumza kupitia runinga moja.

Aliwataka wananchi wazingatie kipimo cha kuweka kila wanapotaka kuchanganya tangawizi, kitunguu swaumu, limao, pilipili kichaa na kitunguu maji ili kuepeka madhara mengine. "Kwa kipindi hiki kuanzia mwaka jana hadi sasa watu wameongeza matumizi ya vitunguu maji, tangawizi, limao, kitunguu swaumu na pilipili kichaa... hivi vyakula ni muhimu hasa unapokuwa na mafua na koo kuwasha ili kuamsha kinga za mwili, ila matumizi yake yawe kwa kiasi," alisema Dk. Subi.

Dk. Subi alisema kitengo cha vyakula na lishe kimepeleka suala la lishe ngazi ya halmashauri ili kuongeza uzalishaji wa nafaka na vyakula vingine vilivyopo katika makundi matano ya vyakula.

"Suala la kinga ni la muhimu sana, kila mtu achukue wajibu wake na afya yake... hata Biblia inasema miili yetu ni hekalu takatifu na tuilinde miili yetu kwa namna yoyote ile ikiwamo kula makundi matano ya vyakula ambayo ni wanga, protini, mboga, matunda, na mafuta," alisema Dk. Subi.

Dk. Subi alisema pamoja na kula makundi hayo ya vyakula, ni lazima watu wafanye mazoezi ya kukimbia, kutembea na kufanya shughuli ya kilimo ili kujenga na kuimarisha miili na akili. Aliwataka wananchi kufanya hivyo mara nne kwa wiki kwa muda wa dakika 30, na kwa wagonjwa wanaojifukiza wasisubiri kuzidiwa ndiyo waende hospitali.

"Kujifukiza ni kuzuri, lakini mtu anapohisi dalili zozote za kuumwa awahi kituo chochote cha afya, mtu anakaa nyumbani amejifukiza vya kutosha anakuja ameshaathirika na magonjwa ya mfumo wa hewa... tunajikuta tunatumia oksijeni nyingi kumrudisha katika hali yake ya kawaida, watu wawahi hospitalini," alisema Dk. Subi.



Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Lindi, Maimuna Pathan (kushoto), akitoa msaada wa sabuni katika wodi ya wazazi, alipotembelea Hospitali ya Wilaya ya Nachingwea, mkoani humo juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watunza kumbukumbu, nyaraka wafundwa

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

WATUNZA kumbukumbu na nyaraka za serikali wametakiwa kuwa waadilifu na wazalendo, na wale wenye tabia ya kutoa siri zilizopo katika nyaraka hizo, wakionywa kuacha mara moja kwani wanatia dosari taaluma hiyo nyeti.

Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Bakari Msulwa, alisema hayo mjini Morogoro wakati akizungumza na watunza kumbukumbu na nyaraka za serikali kupitia chama chao (TRAMPA).

Akasema taaluma hiyo ni muhimu, hivyo wanapaswa kuiheshimu kwa kufanya kazi kwa uadilifu, na wakitumwa kupeleka nyaraka za serikali wasivujishe siri zilizomo au kugeuka sehemu ya waamuzi na kuanza kuzungumza bila ridhaa ya mwajiri. "Tena hii kazi wengi wanaoifanya vijana, mnapaswa kubadilika, mngekuwa mnasababisha siri nyingi kuzagaa ovyo mitaani... ni kinyume cha utaratibu na kukiuka maadili ya kazi zenu," alisema Msulwa.

Mkuu huyo wa Wilaya alisema watunza kumbukumbu na nyaraka wana nafasi kubwa kurahisisha au kukwamisha shughuli kwa kuchelewesha kufikisha nyaraka sehemu husika kwa wakati, hivyo kusababisha jambo kuchelewa kushughulikiwa.

Alisema serikali inatambua mchango mkubwa unaofanywa na watunza kumbukumbu na nyaraka za serikali, na kwamba kila kinachofanyika ofisini kuna mkono wao bila kujali anatoka ofisi gani.

Makamu wa Rais wa TRAMPA, Devota Mrope, alisema wanakabiliwa na changamoto ya waajiri kutotenga bajeti kwa ajili ya kuwalipia watunza kumbukumbu kushiriki mafunzo na mkutano mkuu.

Akasema changamoto nyingine ni waajiri kuendelea kuweka watumishi eneo la ofisi za kumbukumbu wasio na sifa ama wenye matatizo ya kinidhamu kwenye maeneo yao.

Akamwomba mkuu huyo wa wilaya kulisemea hilo kwenye mamlaka za serikali za mitaa ili watambue eneo la masijala ndio kitovu cha taarifa za serikali , taasisi na taifa kwa ujumla hivyo sio sahihi hata kuwapangia kazi watumishi wasio na sifa za kitaaluma ama waliopo na matatizo ya kinidhamu.

Mrope alisema TRAMPA tangu kuanzishwa kwake wameweza kusimamia na kuondoa mwingiliano wa majukumu ya kitaaluma, kukemea vitendo visivyofuata taaluma.

# Kiwanda cha dawa tiba asili kujengwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI inatarajia kujenga kiwanda cha kutengeneza dawa za tiba asili ambacho kitakuwa chini ya Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMRI), huku ikiwataka wananchi kupanda miti dawa kwa wingi ili kukidhi mahitaji ya kiwanda hicho.

Aidha, serikali imesisitiza wananchi kuendelea kutumia dawa za tiba asili ambazo zimesajiliwa na ili kuepuka kupata matatizo ya kiafya.

Hayo yalibainishwa na Mkurugenzi Msaidizi wa Tiba Asili na Tiba Mbadala kutoka Wizara ya Afya, Dk. Paulo Mhame, wakati akielezea umuhimu wa kutumia tiba asili na mbadala kwa ajili ya kujikinga na magonjwa ya mfumo wa upumuaji.

Dk. Mhame alisema ikiwa serikali imehalalisha kutumia tiba asili, ni vema wananchi wakajikita kulima miti dawa ambayo itahitajika kwa ajili ya matumizi ya kutengeneza dawa katika kiwanda ambacho kinatarajiwa kujengwa.

"Tunaomba wananchi wapande miti dawa ambayo inatumika kutengeneza tiba asili na mbadala, ili kiwanda kikianza kusiwe na upungufu wa malighafi zinazohitajika kutengeneza dawa hizo," alisema Dk. Mhame.

Aliitaja baadhi ya miti dawa ambayo inahitajika kupandwa ni malimao, pilipili kichaa, tangawizi, mikaratusi, kivumbasa, vitunguu maji, vitunguu saumu, michaichai na mingine mingi ambayo inahitajika kutengeneza dawa hizo.

Alisema malighafi hizo si kwa ajili ya kutumika nchini pekee, bali duniani kote zinakohitajika kwa ajili ya matumizi mbalimbali kwa binadamu jambo ambalo wakulima watanufaika pia.

"Pamoja na kuwa ni tiba asili, pia jamii itumie fursa kulima kwa wingi vitu hivyo ambavyo ni biashara na vitawasaidia kuwainua kiuchumi," alisema Dk. Mhame.

Akizungumzia kuhusiana na watu kutumia dawa hizo kiholela, aliitaka jamii inapokwenda kununua dawa hizo wahakikishe zimesajiliwa ili kuepuka kupata madhara ya kiafya hapo baadaye.

"Tunaomba jamii iwe makini kununua dawa kiholela kwa ajili ya magonjwa ya mlipuko, muwe mnaangalia usajili wake, lakini kuweni makini na wale wanaotembeza ovyo mitaani dawa hizo."

Alisema waganga wa tiba asili ambao wanatambulika ni 75,000, lakini waliosajiliwa ni 26,950, huku akiwataka ambao bado hawajasajiliwa wafanye hivyo, ili kutambulika.

Hata hivyo, alisema wizara inaendelea kutoa elimu kwa waganga wa tiba asili katika maeneo ya vyuo mbalimbali nchini, lengo ikiwa ni kwenda kujisajili, lakini kuwapa mwongozo wa namna ya kutoa huduma hiyo kwa njia ya sayansi na teknolojia.




Ukurasa 12

**Ujue mkaa mpya ulioingia sokoni kurithi nishati kuni na mkaa wake**



Ukurasa 13

TMDA yahamishia kampeni zake kusaka viwango vitakasa mikono



Ukurasa 14

**Jamii inavyohamasishwa dawa asili ili kuepuka maambukizi ya corona**

# Mahafali ya kwanza Baraza la Wauguzi tangu 1953 ikibeba ya kipekee ya uuguzi

## • Bosi Mkuu wa Uuguzi awasilisha dozi

**Na Yasmine Protace**, KIBAHA

WAKUNGA na wauguzi wanafahamika kuwa watu muhimu katika sekta ya afya, kutokana na kazi wanazozifanya.

Kila hospitali au vituo vya afya, kuna watu wanaojulikana kama wakunga ambao ni mahususi kwa uzazi na wengine wauguzi kwa huduma ya umma.

Serikali inasema kazi yao ni kuhakikisha wanatoa huduma za afya kwa wageni waliofika tu ambao wamefika kupata huduma hiyo.

Ni kauli iliyowasilishwa na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Dk. Dorothy Gwajima, katika hotuba yake iliyosomwa na Mkurugenzi wa Idara ya Uuguzi na Ukunga, Ziada Sellah, kuwasajili wauguzi na wakunga wapya.



Wauguzi wahitimu waliokua katika mahafali yao, Kibaha mkoani Pwani. **PICHA: MTANDAO**

Akizungumza katika katika hafla ya kwanza ya kuwasajili wauguzi na wakunga wapya iliyofanyika kwenye Kituo Cha Maendeleo ya Uuguzi na Ukunga, mjini Kibaha, anasema ni wajibu wao kufanya kazi kwa weledi ili kuhakikisha jamii inanufaika na huduma hizo.

Ziada anasema wanataaluma hao wanapaswa kuzingatia viapo vya taaluma walizonazo na kutoa huduma kwa kujali utu, heshima na upendo kwa wagonjwa wanaowahudumia katika vituo vyao vya kazi.

"Tukio hili litasaidia kutoa msisitizo kwa wanataaluma kutambua wajibu wao katika utoaji wa huduma huku wakizingatia maadili ya taaluma zao.

"Kitendo hiki kilitakiwa kutekeleza kipindi kirefu kilichopita na ni vyema kikatekelezwa na taaluma zote za sekta ya afya nchini, ili kuwafanya wahitimu kuheshimu taaluma zao," anasema.

Katika kuboresha na kutekeleza majukumu ya Baraza la Wauguzi na Wakunga nchini, ziada amelitaka kuzingatia ubora wa stadi na maadili ya taaluma, ili kushuhudia mabadiliko makubwa ya ubora wa huduma za afya nchini.

"Tumeendelea kushuhudia changamoto nyingi za huduma zinazotolewa bila kuzingatia maadili ikiwa ni pamoja na kunyanyaswa wateja, natoa msisitizo tena kwa wanataaluma wote wa sekta ya afya zingatieni viapo vyenu," anasema Ziada.

Sellah amewahimiza viongozi katika ngazi za mikoa na hospitali za rufani, ambazo wamepewa mamlaka na Sheria ya Uuguzi na Ukunga ya Mwaka 2010, kuchukua hatua za awali, panapobainika kuna upungufu katika utoaji wa huduma.

"Tekelezeni majukumu yenu kwa haraka iwezekanavyo na kisha mtoe taarifa kwa Baraza la Uuguzi na Ukunga makao makuu kwa hatua zaidi.

"Wateja wanapenda kushuhudia haki inapatikana mapema, kuchelewa kuchukua hatua panapotokea upungufu kunaleta picha mbaya kwa wateja na kuleta taswira kuwa kuna kulindana au udhaifu katika usimamizi wa maamuzi,"anasema.

Ziada analipongeza baraza hilo kwa kuandaa tukio hilo na kuwahimiza liwe endelevu kwa wanataaluma kuelewa maana ya baraza na majukumu yake, pia akiwasisitiza kuhusu maadili ya taaluma yao.

Mwenyekiti wa Baraza la Uuguzi na Ukunga nchini, Abner Mathube, anasema sheria iliyounda baraza hilo ilitungwa kwa lengo la kuhakikisha Watanzania wanapata huduma za uuguzi na ukunga zilizo salama.

Hivyo, baraza hilo limechukua hatua ya kuhakikisha linawasajili wataalamu wenye sifa za kitaaluma na kuwachukulia hatua za kisheria, wote wanaotoa huduma chini ya viwango vilivyowekwa.

Wakati huo huo Kaimu Msajili wa Baraza la Uuguzi na Ukunga, Happy Masenga, anasema baraza linahakikisha leseni ya kutoa huduma za kitaaluma za uuguzi inatolewa kwa waombaji waliopitia mafunzo yaliyokubalika, kutoka vyuo vinavyotambulika na kufaulu mitihani ya usajili inayoendeshwa na baraza.

Masenga anasema, tangu mwaka 2014, baraza hilo limekuwa likiendesha mitihani ya usajili na leseni, ili kupima umahiri wa wahitimu kwa lengo la kujiridhisha kama wanao uwezo wa kutoa huduma salama kwa wateja na hadi sasa wahitimu 30,715 wamekwishaifanya mitihani hiyo.

Ni mahafali yaliyoandaliwa na Baraza la Uuguzi na Ukunga nchini na yamefanyika kwa mara ya kwanza tangu baraza hilo kuanzishwa mwaka 1953.

Ndani ya hafla hiyo, kuna jumla ya wauguzi na wakunga 839 walihitimu masomo ya uuguzi na ukunga katika ngazi mbalimbali na kufaulu mitihani ya usajili na leseni iliyofanyika Novemba, 2020.

MAZINGIRA

# Ujue mkaa mpya ulioingia sokoni kurithi nishati kuni na mkaa wake

## • Vyuo vya Dar tayari vyaanza nayo

**Na Beatrice Philemon**

KIHISTORIA, sehemu kubwa ya vyanzo vya nishati vimejikita katika mkaa na kuni, Ni hali inayochangia kuharibu misitu na mimea kwa ujumla.

Takwimu kutoka Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), zinaonyesha mahitaji ya nishati ya mkaa nchini yanafikia tani milioni mbili hadi tatu kwa mwaka na ili kuzalisha tani moja ya mkaa, zinahitajika mita za ujazo 10 hadi 12 za miti.

Utafiti wa TFS unaonyesha jiji la Dar es Salaam peke yake, kunaingizwa zaidi ya magunia 500,000 ya mkaa kila mwezi, ikiwa ni kiashiria cha uharibifu wa misitu.

Ni hali inayoshinikiza haja ya mageuzi makubwa kukabili athari dhidi ya vyanzo vya mimea, kwa kuhamia matumizi ya nishati mpya gesi na teknolojia mkaa mbadala, hata kuokoa mazingira, pia nafuu kiuchumi kwa watumiaji.




Jiko sanifu linalotumia mkaa mbadala litakalosambazwa kwa wadau mbalimbali jijini Dar es Salaam, kupunguza matumizi ya mkaa wa kuni. Kulia ni magunia ya mkaa mbadala yakiwa tayari yamezalishwa kwenda kwa wateja. **PICHA ZOTE: BEATRICE PHILEMON**

### IJUE NISHATI MPYA

Hivi sasa kuna teknolojia bora ya nishati ya kupika kupitia mabaki ya misitu na taka za kilimo kuzalisha mkaa mbadala maarufu, ikiwamo majiko sanifu.

Vifaa tajwa ni kuandaa tofali ndogo zitokanazo na kukandamizwa taka za shamba, misitu au viwandani na kutumika kama chanzo cha nishati.

Hapo kuna taka kama randa za mbao, vumbi la mkaa, pumba za mpunga, vipande vya mbao na mashudu.

Meneja, Mradi wa Mashujaa wa Mkaa Mbadala, kutoka Taasisi ya Uongozi na Maendeleo ya Ujasilimali (IMED), Rotildis Massawe, anaiambia Nipashe, teknolojia hizo zinatumika kupunguza matumizi ya mkaa jijini Dar es Salaam.

Kutumia mkaa wa kawaida, maana yake ni kukaribisha ukataji miti katika maeneo mbalimbali, ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, pia ni elimu kwa wanafunzi.

Mdau, kampuni ya Space Engineering katika jitihada za kupunguza utumiaji kaa, imeanzisha mpango maalumu wa kutoa majiko sanifu bure kwa washirika kama Mama Lishe na wakaanga chipsi wa Dar es Salaam, sharti watatakiwa kununua mkaa mbadala kwao.

Pia, inasema imejikita kuhudumia wenye kipato cha chini na kati katika teknolojia ya mkaa mbadala, rai ikienda mbali vyuoni, shule za bweni, hospitali, kambi za jeshi, ili wakabiliane na mabadiliko ya tabianchi.

> **Tunaamini teknolojia hii ya kutengeneza mkaa taka na majiko sanifu itakapoboreshwa itaharakisha maendeleo nchini hasa katika matumizi ya nishati majumbani na kibiashara.**

Hadi sasa, imeshawekeza Sh. milioni 650 kwa ajili ya uzalishaji mkaa mbadala, majiko sanifu na huduma za usafiri na Massawe anasema, kuna jumla ya tani 3398 za mkaa zilizozalishwa kutokana na mabaki ya misitu, taka za kilimo.

Pia, kuna majiko sanifu 650 yaliyokwishatengenezwa na kusambazwa bure jijini Dar es Salaam, katika yake 450 imesambazwa kwenye kantini za Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM), Chuo cha Maji na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam(UDSM) katika hosteli za JPM na DUCE, kote pia wanasambaza mkaa.

Anataja kwingine, ni katika migahawa saba ya UDSM, Chuo Kikuu Ardhi na Chuo cha Maji, wanatumia mkaa mbadala, baada kupatiwa majiko sanifu bure.

Massawe anasema, ni uamuzi uliofikiwa baada ya kubaini jiji la Dar es Salaam, lina watumiaji wakubwa wa nishati mkaa wa kupikia kiwango cha asilimia 70, inayobeba maana ya kubana matumizi ya nishati nyingine na hasa mkaa wa kuni, uliotawala awali, kwa hiyo una manufaa kwa wafanyabiashara wadogo na wakubwa wa vyakula,

Pia, jitihada mbalimbali za kupambana na matumizi ya kuni na mkaa mwaka 2018 kampuni hiyo ilishiriki shindano liitwalo 'Mashujaa wa Mkaa Mbadala' ilijojumuisha kampuni 92 na Space Engineering iliibuka mshindi, ikijitwalia Sh. milioni 200 pamoja na ushauri kutoka taasisi ya IMED.

Akirejea shindano, lilikuwa la kueneza teknolojia bora ya nishati ya kupika kwa mabaki ya misitu na taka za kilimo, kuzalisha mkaa na kukuza nishati mbadala kwenye mazingira endelevu.

"Tunaamini teknolojia hii ya kutengeneza mkaa taka na majiko sanifu itakapoboreshwa itaharakisha maendeleo nchini hasa katika matumizi ya nishati majumbani na kibiashara," anasema

### UHAMASISHAJI WAKE

Shindano hilo liliendeshwa na kampuni ya Shell Exploration and Production Tanzania kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), lengo ni kuhamasisha utunzaji mazingira kitaifa.

"Fedha hizo zilitolewa ili kutumia kuzalisha kwa wingi mkaa mbadala, kupunguza mkaa unaotokana na kukata miti, kukuza ubunifu wa nishati mbadala na mazingira ya biashara, kuanzia vifaa vya kuendesha biashara zao, eneo la biashara, wafanyakazi na taasisi ya IMED kutoa mafunzo kwa wamiliki na wafanyakazi," anasema.

### MTIHANI ULIOPO

"Changamoto tunazokutana nazo sokoni ni nyingi, ila tunajitahidi kupambana nazo kama gesi, kuni, mkaa wa kuni na kadhalika,"anasema Massawe na kufafanua:

"Tunapambana nao kwa kuongeza ubora wa bidhaa yetu, kuwajali wateja, ikiwa ni pamoja na kuwatembelea mara kwa mara kujua kama kuna matatizo na kufanya huduma kwenye majiko yao. Pia tunajitahidi kuhakikisha wateja wanapata bidhaa yetu kwa wakati."

Kwa mujibu wa makakati wao, hivi sasa wahamasishaji hao wanalenga kuongeza uzalishaji mara tatu ya sasa, yaani kutoka tani 4.5 kwa siku hadi tani 13.5 na kuongeza majiko kutoka 450 hadi 1500 kwa mwaka.

Pia, kutazalishwa majiko madogo majumbani kutoka mapya kufikia idadi 1000 kwa mwezi na huduma za kunadi bidhaa hizo.

### FAIDA ZILIZOPATIKANA

Ofisa Mtendaji Mkuu wa taasisi ya IMED, Dk. Donath Olomi, anasema mkaa mbadala hutofautiani mwonekano na umbo kulingana na taka zilizotumika kutengeneza na jinsi ilivyotengenezwa.

"Mkaa huu una faida nyingi ukilinganisha na mkaa wa kawaida, kwa sababu ina nishati joto kubwa kuliko kuni au mkaa wa kawaida na huwaka kwa muda mrefu,"akifafanua kuwa, hauna moshi wala vumbi jingi, hali inayolinda mazingira.

Nishati inapaswa kutumia kijiti kikavu, mafuta ya taa inayochanganywa na mkaa wa kawaida, ili uwahi kuwaka.

Wakati wa mapishi, mtu unapaswa kutumia jiko lenye mlango wa hewa ulio wazi na kuwekewa kifaa 'brikweti' na sufuria lake halizimiki.

Kifaa hicho kinawekwa juu ya chombo cha bati na kinabebwa taratibu kuzuia kunyofoka kufikia ngazi ya jivu, wakati wa kubeba.

Mbali na hilo, mtu hapaswi kuvuruga wala kupondaponda 'brikweti' wakati wa kupika, bali atumie majivu kama nishati, kwa maana linatoa joto jingi.

Pia, kunaelezwa haja ya busara kutumiwa majivu kama mbolea au kifusi cha kujaza vibonde jirani, mahali mtu anakopika. Kitaalamu, inashauriwa, mtu anatakiwa kupangilia mapishi vizuri, katika vyakula vinavyochukua muda mrefu.

"Funika 'brikweti' inayowaka kwa majivu ili isichomeke haraka, uweze kutumia tena baadae," anasema, na kuongeza wanaopika mlo kama wali au pilau, waweke bati juu ya mfuniko wa sufuria kukausha, pia asimwage maji ovyo wakati wa kupika.

Hadi sasa watengenezaji maarufu wanapatikana Mafinga, Iringa, Tabora na Kigoma na Dar es Salaam.

AFYA

# TMDA yahamishia kampeni zake kusaka viwango vitakasa mikono

## • Mwanza 'kumekucha' maabara ya kisasa

**Na Devota Mwachang'a,** MWANZA

MATUMIZI ya vipukusi vitakasa mikono maarufu kama 'sanitizer' kama njia mbadala ya kutakasa mikono katika mahali pasipokuwapo na huduma ya maji na sabuni.

Hivi karibuni kulivyozuka adha ya homa kali ya mapafu inayosababishwa na virusi vya corona nchini, wataalamu wa afya wanashauri hatua ya kwamba ni kuzingatiwa kila mara kukabiliana na usambaaji maambukizi hayo.

Kaimu Mkuu wa Maabara ya Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) Kanda ya Ziwa, Bugusu Nyamweru, ana ufafanuzi kwamba matumizi ya vipukusi visivyo na ubora katika vitakasa mikono, yanahatarisha zaidi afya ya mtumiaji.

Ni matokeo yanayoangukia kwa mhusika kujisikia kichefuchefu, kutapika, maumivu ya kichwa, uoni hafifu, upofu wa kudumu, kifafa, kukosa fahamu, uharibifu wa kudumu kwa mfumo wa mawasiliano mwilini (neva), kuunguza mikono au hata kifo.

### VINAVYOTENGENEZWA

Nyamweru anasema, baadhi ya vipukusi vya kutakasa mikono, sehemu ya malighafi ya kuvitegeneza vina 'vilevi' kwa kazi maalumu ya kuua kabisa au kupunguza viini vya bakteria, ili kulinda afya ya binadamu mtumiaji.

Anataja mifano ya baadhi ya vipukusi vinavyotengenezwa viwandani ni kama hydrogen peroxide, iodine na methylated spirit.

"Wenye viwanda vinavyotengeneza malighafi ya kutengeneza vitakasa mikono (sanitizer), wazalishaji pamoja na wadau wengine wana jukumu la kushiriki katika kulinda afya za watumiaji wa bidhaa zao," Bugusua anasema

Kwa namna gani? Anaendelea: "Kwa kuwafikishia zile zilizopimwa maabara na kuthibitishwa na mamlaka husika (TMDA) kuwa ni nzuri na haziathiri afya ya binadamu."

Akizungumza katika eneo la Buzuruga, kunakolengwa kuwapo maabara mpya ya TMDA jijini Mwanza hivi karibuni, Nyamweru anasema kuna maabara yenye mashine na vifaa vya kutosha vya kisasa, kuchunguza vipukusi, wapimaji na wataalamu.

"Sampuli za vitakasa mikono, lazima zipimwe kwa umakini kutokana na matumizi ya bidhaa hiyo, hasa maeneo ya utoaji huduma ya afya. "Zipo ambazo zinalazimika kuzimuliwa, ili kupata kiwango kinachohitajika kwa matumizi, mfano kusafishia vidonda, mabenchi, kuta na vifaa vingine, lakini lazima ziwe na ubora," anasema Nyamweru.



Matumizi ya vitakasa mikono katika daladala. **PICHA: MTANADAO**




Kaimu Mkuu wa Maabara ya Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) Kanda ya Ziwa, Mwanza Bugusu Nyamweru, akielezea namna mashine maalumu ya kisasa maabara, inavyofanya kazi kwenye vitakasa mikono. **PICHA: DEVOTA MWACHANG'A**

> **Wadudu kwenye 'incubator' huota baada ya saa 24 mpaka 48 kama vile bakteria, lakini fangasi huchukua siku tano.**

Pia, anafafanua kuwa maabara ya Kanda ya Ziwa ikiwa ndani ya miezi mitatu, imeshauchunguza sampuli 102 za vipukusi, vikiwamo vitakasa mikono vinavyotumika hospitalini.

Kaimu Mkuu wa TMDA anasisitiza kwamba vipukusi visivyokidhi viwango, vinachangia kuendelea kuwapo magonjwa yatokanayo na bakteria, kwa sababu wadudu hawafi.

Anasema: "Uhitaji wa 'sanitizer' (vipukusi) unaongezeka kwa wateja wa bidhaa hiyo. Ni pamoja na wajasiriamali wadogo, viwanda na kwa matumizi ya familia nyumbani.

"Sisi wataalamu tunaendelea kuboresha uchunguzi wa vipukusi Ili uwe katika kiwango cha juu, tunawashauri na kuwakaribisha Watanzania kuitumia maabara hii kwa matokeo mazuri na ya uhakika."

### MCHUNGUZI WA TMDA

Jovinary Rwezahura, mchunguzi kutoka Maabara ya TMDA Kanda ya Ziwa, anaeleza ili kitakasa mikono kiwe na uwezo wa kuua viini vya bacteria, ni lazima kuwa na kiwango cha kileo chenye kufikia asilimia 60.

Katika hilo anasema, hiyo inafanya upimaji kupata umuhimu wa kufanyika upimaji kujidhihirisha namna kiwango hicho kimefikiwa kabla hata ya kuruhusu bidhaa kuingia sokoni.

Rwezahura anasema: "Tunafanya upimaji kutathmini na kuangalia ubora wa kiwango cha kilevi kinachopatikana katika kitakasa mikono kwa kutumia mashine maalumu ya kisasa inayoitwa 'Steam Distillation Unit'. Kilevi kinachopimwa ndiyo kiambata muhimu kinachotumika kuua viini vya bacteria au vijidudu."

Anasema, ili kuhakikisha ubora wa vipukusi, ni lazima kuwapo muda maalumu wa kuangalia wadudu waliowekwa wamekufa na tathmini ya muda wao kufikia vifo. Kufaulu ngazi hiyo, ni ishara ya kufaa kwa matumizi ya binadamu.

Waridi Msumari ni Mchunguzi wa Maikbrobailojia (wadudu wadogo) wa Maabara TMDA Mwanza, anayesema kuna njia za kuchunguza vipukusi, lakini zote lazima zifuate hatua ya awali ya kuandaa chakula cha wadudu waliooteshwa (culture media).

Pia, anasema kuna vitenganishi vitakavyotumika kabla ya kipimo cha maikrobailojia kujua uwezo wa sampuli kuua vimelea au kupunguza wadudu waliokusudiwa.

Anasema, upimaji ndani ya maabara ya maikrobailojia wadudu na kipukusi huchanganywa pamoja kwa kwa dakika 10, kisha mchanganyiko huo huwekwa kemikali maalum, kabla ya tathmini iwapo imefanya kazi ya kuua vijidudu.

Mtaalamu huyo anafafanua kuwa sampuli iliyochanganywa na wadudu waliooteshwa huwekwa kwenye kifaa maalumu mithili ya sahani na kuingizwa kwenye mashine ya atamizi inakoachwa kwa muda maalumu, kabla ya kuangalia kama wadudu wameota au la.

Anasema, wadudu kwenye 'incubator' huota baada ya saa 24 mpaka 48 kama vile bakteria, lakini fangasi huchukua siku tano.

### MKUU WA MAWASILIANO

Meneja Mawasiliano na Elimu kwa Umma TMDA, Gaudensia Simwanza, anaeleza kwamba kabla ya mashine hiyo ya 'Steam Distillation Unit' kununuliwa, wachunguzi walitumia mashine iitwayo 'refractometer' ambayo ufanisi wake pia ulikuwa mzuri.

Gaudensia kuwapo uhitaji mkubwa wa bidhaa ikanunuliwa yenye uwezo mkubwa zaidi, akifafanua:

"Kwenye Maabara yetu ya Dar, sampuli zilipimwa kama kawaida na 'refractometer' ambayo ilikuwa inapima lakini majibu yake yalikuwa yanatoka baada ya dakika 10, lakini hii inayotumika sasa inapima na kutoa majibu sahihi ndani ya dakika nne."

Anakumbusha kwamba hitaji la vitakasa mikono haliishi kwa matumizi kukabiliana na ugonjwa corona, bali ni la kila siku katika afya.

MAKALA MAALUM

# Jamii inavyohamasishwa dawa asili ili kuepuka maambukizi ya corona

Na Romana Mallya

JANGA la virusi vinavyosababisha ugonjwa wa Corona (COVID-190 lilipotangazwa mara ya kwanza, dunia nzima ilitaharuki na hata wengine kudhani kuwa ndio mwisho wa maisha yao.

Hata hivyo, tangu kuibuka kwa janga hilo Aprili, mwaka jana, serikali za nchi mbalimbali, ikiwamo Tanzania zilichukua hatua kuhakikisha zinapambana na janga hilo.

Serikali ya Tanzania kwa upande wake, iliwataka wananchi kuchukua tahadhari dhidi ya maambukizi kwa kukaa umbali wa mita moja kutoka mtu mmoja hadi mwingine, kuvaa barakoa, kunawa mikono kwa sabuni na maji tiririka.

Sambamba na hiyo, iliwataka watu kujiepusha na mikusanyiko kama vile misiba, mikutano, ibada na maeneo yenye watu wengi kama vile sokoni na vituo vya mabasi. Kama vile haitoshi, ilichukua uamuzi mgumu wa kufunga kwa muda usiojulikana shule na vyuo.

Hatua zingine zilizochukuliwa ni kuwataka watu kujifukiza, maarufu kama nyungu, pamoja na kutumia dawa asilia katika kupambana na COVID- 19. Hilo ndilo limekuwa likisisitizwa na kupewa kipaumbele zaidi.

Mkurugenzi wa Kuratibu na Kukuza Utafiti kutoka Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR), Dk. Paul Kazyoba, anazungumzia umuhimu wa matumizi sahihi ili kupunguza madhara yanayoweza kujitokeza. Uhamasishaji huo umekuwa ukisisitizwa tangu kutangazwa kwa janga hilo ili kusaidia kuongeza kinga za mwili au kutibu maradhi.

Akizungumza na Nipashe katika mahojiano maalum yaliyolenga kufahamu matumizi sahihi ya tiba asili ili kupunguza madhara yanayoweza kutokea endapo zitatumiwa holela, Dk. Kazyoba anasema ni lazima wananchi wajiridhishe kwanza kabla ya kuzitumia.

Anafafanua kuwa ni lazima mtumiaji ajiridhishe tiba asili anayoitumia kama zimesajiliwa na Baraza la Tiba Asili na kuthibitishwa na Mkemia Mkuu wa Serikali. Anasema kuna idadi kubwa ya wataalamu wa tiba asili nchini na miongoni mwao wako waliosajiliwa na wengi hawajasajiliwa na baraza.

"Kwa mfano kwenye dharura ya ugonjwa wa corona au mlipuko mwingine wowote, ukiangalia kuna dawa nyingi zimesajiliwa na baraza ili zitumike na kuna idadi kubwa ya watu wanajitangaza kuuza dawa zao," anasema.



Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima (wa pili kushoto), akishiriki uchanganyaji wa mazao na mimea mbalimbali kwa ajili ya utengenezaji wa dawa asili. Kulia ni naibu wake, Dk. Godwin Mollel. **PICHA: MTANDAO**

Hata hivyo, Dk. Kazyoba anasema matatizo wanayoyaona watafiti pengine na madaktari wanayazungumza kila mara ni kwamba tiba asili ni huduma yenye fursa duniani na watu hujipatia kipato, hivyo lazima kutakuwapo na wataalamu wa tiba asili ambao ni 'feki'.

"Wanajaribu kukopi (kunakili) dawa za wenzao na kuziwekea ladha nyingine na kuziweka sokoni ili wapate fedha. Hii ndiyo hatari kubwa ninayoiona.

"Jambo la msingi tunashauri watumiaji kabla ya kuzitumia wapate maelezo ya kina kutoka kwa wataalamu wa tiba asili au wauzaji. Hakuna dawa iliyotengenezwa na kutokuwa na maangalizo," anasema.

Anasema kutoa huduma ya tiba asili inayozingatia vigezo au sheria ya tiba asili, tiba mbadala na miongozo ya Baraza la Tiba Asili, inabaki kuwa msingi katika kuhakikisha zinakuwa salama na tija kwenye kutibu magonjwa.

"Mambo wanayotakiwa kufanya ni kujisajili kwenye baraza ukisajiliwa vipo vigezo ambavyo vinaangaliwa, watakagua unakotengenezea dawa, uandaaji wake, namna unavyozifungasha na kuzitoa," anasema.

Mtafiti huyo anasema kuna umuhimu wa wataalamu wa tiba asili kusimama katika miongozo ya baraza na sheria ili kuhakikisha watumiaji wanakuwa salama.

Ili dawa ithibitike kuwa salama, mtaalamu wa tiba asili anatakiwa aipitishe kwa Mkemia Mkuu wa Serikali ili iangaliwe kemikali iliyomo kama ni salama kwa matumizi ya binadamu.

Dk. Kazyoba anasema utafiti unaonyesha wagonjwa wengi walioonwa na wataalamu wa afya mara nyingi hukutwa wanatumia dawa za kisasa na za tiba asili.

"Dawa za tiba asili zinatokana na mimea. Ni dawa chache ambazo kama zimetengenezwa kwa uaminifu na kuzingatia miti dawa ambayo ni salama zinaweza kuleta shida," anafafanua.

Mtafiti huyo anataja matatizo yaliyopo kuwa ni dawa nyingi za tiba asili hazijawahi kufanyiwa utafiti na kuona zikitumika na dawa za kisasa ni athari zipi zinaweza kutokea na kusisitiza kuwa ni vizuri mgonjwa kama amekwenda kwenye matibabu ya kisasa, amweleze daktari wake kama ana matumizi mengine ya tiba asili.

Dk. Kazyoba alitolea mfano dawa lishe ya NIMRCAF ambayo imetengenezwa na NIMR na kueleza kuwa mtu akiitumia na dawa yoyote ya kisasa kwa sababu asilimia 100 ni chakula, haina shida.

"Dawa hii ya NIMRCAF inapoingia ndani ya mwili kufanya kazi kwa haraka sana inawezekana ikaisaidia dawa yako. Ila ziko dawa nyingine ambazo zinatakiwa kuingia kwenye mfumo wa mwili taratibu, hivyo mtumiaji wa NIMRCAF lazima awe makini. Akinywa dawa yake akae saa moja au tatu ndipo anywe NIMRCAF," anaelekeza.

Kwa mujibu wa Dk. Kazyoba, ziko dawa za kisasa ambazo mtumiaji akitumia hukaa kwenye mfumo wa damu muda mrefu, hivyo inapochanganywa na zinazofanya kazi haraka, huaribu mtiririko wa tiba.

Mtafiti huyo anabainisha kuwa kuna utafiti uliofanyika ambao ulilenga kuangalia kabla mtu hajaenda hospitalini huanzia wapi. Katika utafiti huo, anasema yako machapisho ya kisayansi yameonyesha kama una wagonjwa 100, asilimia 55 mpaka 60 ndio huenda hospitalini kupata tiba.

Anasema matumizi ya tiba asili na dawa za kisasa kwa mgonjwa imekuwa ni jambo la kawaida na kwamba yote bado yanahitaji utafiti wa kina ili kulisaidia Baraza la Tiba Asili kutoa miongozo.

**WITO**

Dk. Kazyoba aliwashauri wananchi kabla ya kununua dawa yoyote waulize maswali kuhusu usalama, tija ya dawa husika na kama baraza inaifahamu.

"Kama ni miti chakula dawa itakuwa salama, lakini kama ni miti dawa inatakiwa ujiridhishe kwanza usalama wake, sheria ya tiba asili na tiba mbadala ya mwaka 2002 iliwekwa lengo ni kuhakikisha tiba asili inaendelezwa ili kuchangia kwenye sekta na pato la taifa, lakini lazima usalama wa watumiaji usingatiwe," anasema.

Anasema usalama unatakiwa kuzingatiwa kwa sababu tiba asili ni fursa na kwamba wapo watakoitumia kufanya utapeli kwa kutengeneza mchanganyiko na kuweka nembo na kuuza.

"Baraza limefanya kazi kubwa ya kuhamasisha na wamesajiliwa watu wengi ili kuhakikisha matumizi sahihi ya tiba asili Tanzania yanakuwapo na siziwe chanzo cha matatizo mengine," anasema.

Mtafiti huyo anasema dawa za vimiminika zisipoandaliwa kwenye mazingira rasmi zina hatari kusababisha matatizo mengine kwa sababu ya vimelea vya bakteria na fangasi vinaweza kumea humo ndani kwa urahisi.

**MATUMIZI KWA WATOTO**

Dk. Kazyoba anasema kila dawa ina maelekezo na kama ziko zinazouzwa bila hilo ni tatizo.

"Haijalishi kama ni tiba ya asili au tiba ya kisasa lazima dawa iwe na maelekezo kwa mtumiaji ya nini afanye na nini asifanye, mfano NIMRCAF ina maelekezo watu wazima waitumiaje na watoto kuanzia umri gani inapendekeza wapewe vipi, dawa zote zinatakiwa kuwa na maelekezo na mwongozo wa baraza ndiyo unaelekeza hivyo," anasema.

**ATHARI KIAFYA**

Dk. Kazyoba alikanusha kwamba siyo kweli matumizi ya dawa za tiba asili zinasababisha matatizo ya figo.

Dk. Kazyoba anasema ili kuondoa utata, eneo hilo linahitaji kufanyiwa utafiti ili kujiridhisha kama tiba asili inachangia matatizo ya figo.

"Kuchangia sikatai kwa sababu kama nilivyosema ndani ya sekta hii wajanja wajanja ni wengi ambao wanaweza kuchukua mti wowote akatengeneza dawa.

"Matatizo ya figo yanaweza kusababishwa na mambo mengi mfano ulaji wa dawa za kisasa ovyo ovyo usiothibitiwa. Wataalam wenzangu lazima kufanyike utafiti inawezekana utumiaji dawa holela usiozingatia miongozo ya madaktari nao unaweza ukachangia kwenye matatizo haya tunayoyaona sasa hivi," anasema.

Anasema upo utafiti ambao wanashirikiana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, kuangalia matatizo ya figo visababishi ni nini hasa.

Dk. Kazyoba anasema hayo ni mambo ambayo wanataka kuyafanyia utafiti kwa kuwa sababu ni nyingi, ambapo zipo nyingine wanaziona lakini hawajui kama ndizo zinazochangia matatizo hayo.





# Katibu Mkuu ataka watumishi Viwanda na Biashara kubadilika

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

KAIMU Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Dk. Consolata Ishebabi, amewataka watumishi wa wizara hiyo, kutumia mafunzo ya dhana ya KAIZEN kuongeza tija na ubora katika utendaji kazi na majukumu yao ya kila siku.

Kaimu huyo ambaye ni Mkurugenzi wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo wa Wizara ya Viwanda na Biashara, alisema hayo jijini Dodoma katika ufunguzi mafunzo ya KAIZEN kwa watumishi wa wizara yaliyofanyika katika Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) jijini hapa.

KAIZEN ni neno la kijapani lenye maana ya badilika kwa ubora/uzuri linalohusu shughuli endelevu zinazofanyika ili kuboresha kazi katika mifumo michakato na nyanja yoyote ya kuendesha biashara na asili yake ni Japan na sasa inatekelezwa duniani kote.

Alisema mafunzo hayo yanalenga kuwawezesha watumishi wa wizara kubadili mtazamo, kuongeza tija, uwajibikaji na ubora mahala pa kazi.

"Tuiweke KAIZEN katika mipango yetu kuanzia ofisini hadi katika familia zetu ili kuongeza tija na ubora katika utendaji kazi na maisha yetu ya kila siku na tujipime kwa kutumia vipimo vya utumishi kama OPRAS," alisema Dk. Ishebabi.

Alisema mafunzo hayo pia yanalenga kuongeza ufahamu kuhusu mfumo wa falsafa ya uongezaji thamani endelevu wa tija na ubora viwandani ili kushiriki kikamilifu katika kufanikisha utekelezaji wa falsafa hiyo katika sekta wanazozi hudumia.

Dk. Ishebabi pia alisema mafunzo hayo yanaongozwa na kaulimbiu isemayo "KAIZEN kwa Tanzania ya Viwanda Shindani kwa Maendeleo Shirikishi".

Kadhalika, alisema kaulimbiu hiyo inaendana na azma ya serikali ya awamu ya tano inayodhamiria nchi kuwa na uchumi wa kati wa viwanda ifikapo mwaka 2025.

Mradi wa KAIZEN unaofadhiliwa Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Japan (JICA), unalenga kuongeza tija na ubora katika sekta ya viwanda na shughuli za maisha ya kila siku inaongozwa na misingi ambayo iko katika ubunifu wa mawazo, maarifa na ushiriki wa kila mtu ndani ya taasisi, shirika au kampuni.



Mwenyekiti wa Chama cha Walinzi Binafsi Kanda ya Kati Dodoma (TSIA), Lukanus Kayombo (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma. Kulia ni Mhasibu Msaidizi wa TSIA, Kanda ya Kati, Fidelis Luhunya. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# 'Fire Clubs' zapunguza majanga ya moto

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

JESHI la Zimamoto na Uokoaji limesema uwapo wa klabu za wanachama wa jeshi hilo (Fire Club) umesaidia kutoa elimu kwa wanafunzi na jamii na kupunguza kwa kiasi kikubwa majanga ya moto shuleni na katika jamii.

Hayo yalibainishwa jana na msemaji wa jeshi hilo, Inspekta Joseph Mwasabeja, wakati akizungumza na Nipashe kuhusu kufungua klabu hizo katika shule za msingi, sekondari na vyuoni.

Inspekta Mwasabeja alisema uwapo wa klabu hizo katika maeneo hayo, umesaidia kuwapa uelewa wanafunzi namna ya kukabiliana na majanga ya moto na mengine yanayotokea katika maeneo wanayoishi.

Alisema hadi sasa wana 'Fire Club' 786 zenye wanachama 34,018 katika mikoa yote huku Dodoma wakiwa na klabu 13 zenye wanachama 914 ambazo ziko katika shule za sekondari na msingi.

Alisema lengo ni kutoa elimu kwa wanafunzi hao ambao wako bweni na wale wa shule za kutwa ambao hawakai mabwenini na wamekuwa wakisaidia kutoa elimu kwa ndugu, jamaa na marafiki walioko katika maeneo mbalimbali wanayoishi.

Pia alisema wanaklabu hao wanapohitimu masomo yao, kutokana na mafunzo waliyopata kutoka jeshi hilo huwapatia vyeti na kuendelea kuwafuatilia katika maeneo waliyoko ili kutoa elimu katika jamii inayo wazunguka.

Sambamba na hilo, alisema wametengeneza uhusiano na skauti ambao wamekuwa wakitoa taarifa ya majanga yoyote ya moto.

"Tumekuwa tukiwatumia skauti katika shule ili kutupa taarifa haraka endapo kuna viashiria vya moto katika eneo la shule, hivyo atatumika kama mtoa taarifa wa kwanza," alisema Mwasabeja.

Kuhusu ujenzi wa makazi ya askari wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Mwasabeja alisema unaendelea na uko katika hatua nzuri kwa kuwa yanatakiwa maghorofa manane. Kati ya hayo, sita yako kwenye hatua za mwisho na mengine mawili yanaendelea kujengwa.

"Rais John Magufuli alitoa Sh. bilioni tano kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za askari wetu, hivyo utakapokamilika wataenda kukaa kwani uhitaji uliopo ni mkubwa, lakini kila ghorofa litachukua familia ya watu 10," alisema Mwasabeja.

Akizungumzia ujenzi wa vituo vya zimamoto na uokoaji, alisema maeneo mbalimbali wameshapata viwanja lakini katika Jiji la Dodoma tayari kuna kituo cha kisasa kimejengwa katika wilaya ya Chamwino na wanatarajia kuanza kwa ujenzi wa kituo cha kisasa katika eneo la Nzuguni.

# Aishauri serikali kununua, kuhifadhi dawa za magonjwa ya mfumo wa hewa

**Na Paul Mabeja**, DODOMA

MWENYEKITI wa Chama cha Walinzi wa Sekta Binafsi (TSIA) Kanda ya Kati, Lukanus Kayombo, ameishauri serikali kununua na kuhifadhi katika bohari yake dawa zote za tiba asili zilizothibitishwa na mamlaka husika kuwa zinatibu magonjwa ya mlipuko yatokanayo na mfumo wa hewa.

Kayombo aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari namna ambavyo kampuni za ulinzi sekta binafsi Kanda ya Kati zinavyochukua tahadhari kujikinga na magonjwa ya mlipuko.

Alisema kutokana na dawa za tiba asili ambazo zimekuwa zikielezwa kutibu magonjwa hayo bei zake kuwa juu hali ambayo inawanyima wananchi wa hali ya chini kuzimudu.

"Naishauri serikali kutokana na kuwa imekuwa ikitutangazia kuwa dawa za asili ambazo zinatibu magonjwa haya zipo ambazo tayari zimethibitishwa na mamlaka husika, basi kupitia wizara yake ya afya wazinunue na kuziweka katika bohari yao na wao ndiyo waziuze kwa wananchi kwa gharama nafuu," alisema.

Hali hiyo, Kayombo alisema itasaidia watu wengi kuzipata dawa hizo ambazo zimekuwa zikishauriwa kutumiwa na viongozi wakuu wa nchi.

Akizungumzia kampuni binafsi za ulinzi ambazo zimekuwa zikichukua tahadhari, alisema hivi sasa wanatoa elimu kwa wafanyakazi namna ya kujikinga dhidi ya magonjwa hayo.

"Sisi hapa lazima ukute maji ya kunawa na sabuni, vitakasa mikono lakini tumegawa barakoa kwa walinzi wote na kila wanapoingia na kutoka hapa tunawapima joto lao la mwili," alisema Kayombo.

Pia alisema pamoja na kuchukua tahadhari hizo, lakini wamekuwa wakitoa ushauri kwa walinzi kuhakikisha wanazingatia maelezo ya serikali katika matumizi ya tiba asili pamoja na kujifukiza.

"Dawa hizi zipo toka siku nyingi sema tu watu walikuwa hawazifuatilii. Kutokana na serikali kuzitambua sisi tunashauri wazitumie kwa wingi dawa hizi pamoja na kujifukiza kama inavyoelekezwa na wizara husika," alisema.

Hata hivyo, aliwataka waganga wa tiba asili nchini ambao wamekuwa wakidai kuwa wanazodawa za kutibu magonjwa hayo ya mfumo wa kupumuia wajitokeze na kujisajili katika mamlaka husika ili watambulike kisheria.







Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, mkoani Mbeya, ambaye ni Diwani wa Ikimba, Katule Kingamkono (wapili kulia), akiwa na viongozi wa kitongoji cha Ibungu, wakati wakikagua eneo la ujenzi wa Zahanati ya Ibungu, jana. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Urasimu wakwamisha uanzishaji viwanda

**Na Nebart Msokwa,** BUSOKELO

VIKUNDI vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu wanaonufaika na mikopo ya asilimia 10 ya mapato ya ndani katika Halmashauri ya Busokelo mkoani Mbeya, vinashindwa kuanzisha viwanda vya kusindika bidhaa za vyakula kutokana na urasimu wa taasisi zinazosimamia shughuli hizo.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri hiyo, Agnes Elikunda, aliyasema hayo juzi wakati wa kutoa mkopo wa Sh. milioni 133 kwa vikundi 25 vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Mikopo hiyo ilikabidhiwa na Mbunge wa Busokelo, Atupele Mwakibete.

Alisema vikundi hivyo vinahitaji kuanzisha viwanda vidogo vya kusindika vyakula, lakini kutokana na urasimu wa taasisi hizo, wenye vikundi wanakata tamaa na kuamua kufanya shughuli zingine.

"Vikundi vingi havina miradi yenye mwelekeo wa viwanda kutokana na tatizo la urasimu ambao vinakutana nao kwa wahusika wanaosajili shughuli hizo. Lakini tunaendelea kutoa elimu na kuhamasisha ili waendelee kupambana," alisema Elikunda.

Pia alisema vikundi vingi vimekuwa vikiomba mikopo hiyo, lakini vinakosa sifa za kukopesheka hasa vijana na watu wenye ulemavu na kwamba vikundi vya wanawake havina tatizo kubwa.

Vikundi vya vijana. Alisema huwa havikidhi vigezo vya kukopeshwa kutokana na wengi kuwa na umri wa zaidi ya miaka 35 unaohitajika kisheria na kwamba wenye ulemavu pia wanakosa sifa kwa sababu wanaunda vikundi lakini wanakuwa hawafahamiani vizuri.

Akikabidhi mkopo huo kwa vikundi hivyo, Mwakibete aliwataka wanufaika wa mikopo hiyo kuirejesha kwa wakati ili vikundi vingine vinufaike kama ambavyo inatakiwa kwa mujibu wa sheria.

Alisema kwa vikundi vya vijana ambavyo havinufaiki na mikopo hiyo kwa sababu ya kigezo cha umri, wataunganishwa na taasisi za fedha ili wakopeshwe huko na waendeshe shughuli zao kwa faida na kuboresha maisha yao.

Pia alisema ziko fedha ambazo zinatoka katika Mfuko wa Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na zinazotoka kwenye mashirika ya kimataifa ambazo zinatakiwa zinufaishe vikundi hivyo lakini halmashauri haijawahi kunufaika nazo.

"Waziri Mkuu atafanya ziara jimboni kwetu mwezi ujao. Sasa mimi kama mbunge wenu kazi yangu itakuwa kumkumbusha ili na sisi tunufaike. Lakini fedha hizi mnazopewa si hisani mtatakiwa kuzirejesha," alisema Mwakibete.

Aliongeza kuwa fedha hizo endapo wanufaika watazitumia vizuri, zitawafanya kuwa matajiri na endapo watazitumia ovyo wataendelea kuwa maskini.

Baadhi ya wanufaika wa mikopo hiyo waliishukuru serikali kwa kuanzisha utaratibu huo kwa madai kuwa umewasaidia kuboresha maisha yao kwa kujiinua kiuchumi.

Mmoja wa wanufaika hao, Ikupasya Mwakasege, alisema kutokana na mikopo hiyo amesomesha watoto wake ambao mmojawapo anasoma Chuo Kikuu na kwamba ana biashara ambayo inamwezesha kuendesha maisha yake na kurejesha mikopo.

# Madiwani wapitisha bajeti bilioni 33.9/-

**Na Grace Mwakalinga,** KYELA

BARAZA la Madiwani katika Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, limepitisha rasimu ya bajeti ya Sh. bilioni 33.9 kwa mwaka wa fedha 2021/22 kwa ajili ya miradi mbalimbali ya maendeleo.

Akisoma rasimu hiyo juzi mbele ya Baraza la Madiwani, Ofisa Mipango wa Halmashauri, Francis Mwaipopo, alisema fedha hizo zimeelekezwa katika mishahara ya watumishi, ujenzi wa miundombinu kwenye sekta ya elimu, afya na maji.

Alisema endapo rasimu hiyo ya bajeti itapitishwa, itachochea maendeleo katika wilaya hususani kukamilisha mradi wa maji ambao utahudumia wananchi wote kwa kuwa watakuwa na uhakika wa kupata majisafi na salama ya bomba kulinganisha na ilivyo sasa.

"Rasimu hii ya bajeti ambayo imepitisha fedha Sh. bilioni 33.9 imehusisha masuala mbalimbali ikiwamo mishahara ya watumishi, miradi mbalimbali ya maendeleo, mapato ya ndani, ruzuku na matumizi mengineyo," alisema Mwaipopo.

Hata hivyo, alisema makisio ya mapato ya vyanzo vya ndani kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ni Sh. bilioni 3.883 ikiwa ni ongezeko la asilimia moja ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2020/21.

Akizungumzia rasimu hiyo, Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, Claudia Kitta, aliwasihi wataalamu na madiwani kushirikiana, ili kukamilisha miradi mbalimbali ya maendeleo na kufikia malengo yaliyowekwa katika rasimu hiyo ya bajeti.

Alisema fedha zilizoelekezwa kwenye miradi zisimamiwe kikamilisha na kupunguza matumizi yasiyo na ulazima.

Mwenyekiti wa Halmashauri, Katule Kingamkono, alisema wananchi wanatarajia kupata maendeleo

# Chalamila akagua miradi ya maji iliyotelekezwa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, ameanza kukagua utekelezaji wa miradi ya maji wilayani Mbarali ambayo hivi karibuni Naibu Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi, aliagiza itekelezwe haraka kutokana na kutelekezwa muda mrefu.

Chalamila alianza ziara hiyo juzi kwa kutembelea miradi miwili ya Ruduga-Mawindi na Ilongo Group ambako kwa sasa mafundi wanaendelea kujenga matangi ya kuhifadhia maji, kuchimba mitaro na kulaza mabomba.

Aliwataka mafundi hao kujenga matangi hayo kwa kuzingatia viwango ili idumu kwa muda mrefu na isije ikasababisha madhara kwa wananchi endapo matangi hayo yataporomoka.

Aidha, aliwataka watendaji wa Wakala wa Maji Mijini na Vijijini (RUWASA) kuendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu utunzaji wa mazingira ikiwamo vyanzo vya maji.

"Vifaa hivi tunzeni vizuri na hakikisheni mnawashirikisha wananchi ili visije vikaibiwa, lakini hakikisha hakuna wizi wa fedha za umma kwenye miradi hii," alisema Chalamila.

Chalamila aliomba ushirikiano wa mikoa mitatu ya Mbeya, Iringa na Njombe kwenye utunzaji wa vyanzo vya maji ili kuhakikisha wananchi wananufaika na maji hayo na pia yanalinufaisha taifa kwa kupeleka maji kwenye miradi mikubwa ya umeme iliyoko katika Bonde la Mto Rufiji.

Aliiagiza halmashauri kuhakikisha maji ya mradi wa Ruduga-Mawindi unainufaisha pia Shule ya Sekondari Mawindi ambayo itakuwa inachukua idadi kubwa ya wanafunzi.

Akizungumza wakati wa ukaguzi wa mradi wa Ruduga- Mawindi, Meneja wa RUWASA Wilaya ya Mbarali, Mhandisi Samwel Hechei, alisema mradi huo unatekelezwa kwa kutumia akaunti 'Force Account' na kwamba utaratibu huo umesaidia kupunguza gharama.

Alisema awali mradi huo ulikuwa unakadiriwa kutumia gharama ya Sh. bilioni 12.38, lakini kwa sasa unatekelezwa kwa gharama ya Sh. bilioni 8.56 na kwamba fedha hizo zinatokana na mfuko wa maji.

Mradi huo ukikamilika, alisema utanufaisha vijiji vya Ipwani, Matemela, Mkandami, Manienga, Itipingi na Kangaga na kwamba unatekelezwa chini ya usimamizi kutokana na kukwama kwa muda mrefu.

"Mradi huu ni muhimu sana kwa wananchi wa vijiji hivi, utasaidia kupunguza magonjwa yatokanayo na matumizi ya maji yasiyokuwa safi na salama, lakini utasaidia kuchochea shughuli za maendeleo kwa sababu wananchi watapata maji jirani na makazi yao," alisema Hechei.

Meneja wa RUWASA Mkoa wa Mbeya, Mhandisi Vivian Mndolwa, alisema watahakikisha miradi yote inatekelezwa kwa viwango vinavyostahili.

Alisema Mradi wa Ilongo Group alisema unatekelezwa kwa gharama ya Sh. milioni 846.7 na kwamba ukikamilika utasaidia kupunguza tatizo la maji kwenye vijiji vyote vinavyolengwa kwenye mradi huo.

Mwishoni mwa Desemba, mwaka jana, Naibu Waziri wa Maji, Mahundi, alifanya ziara katika wilaya zote za mkoa wa Mbeya na kuonyesha kukerwa na utekelezaji mbovu wa miradi ya maji katika wilaya ya Mbarali.





# Kiwanda cha kusindika dagaa kujengwa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Abdalla Hussein Kombo, amesema Serikali ya Zanzibar inakusudia kujenga kiwanda cha kusarifu dagaa katika eneo la Fungurefu mkoa wa Kaskazini Unguja ikiwa sehemu ya mikakati ya kuwawezesha wajasiriamali wadogo kupiga hatua katika maendeleo ya kiuchumi.

Aliyasema hayo jana, katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akitoa ufafanuzi kuhusu mikakati ya serikali kuingia katika uvuvi wa uchumi wa buluu.

Waziri alisema Shirika la Uvuvi la Zanzibar (ZAFICO) linakusudia kutekeleza miradi mitatu ikiwa ni sehemu ya mikakati ya uvuvi wa uchumi wa buluu pamoja na ujenzi wa kiwanda cha kusarifu dagaa.

Alisema mradi mwingine ni kiwanda cha minofu ya samaki pamoja na ufugaji wa vifaranga vya samaki na majongoo ya pwani.

"Hiyo ni miradi mitatu ambayo inatekelezwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia ZAFICO kwa mkopo wa Shirika la Kimataifa la Maendeleo ya Kilimo (IFAD)," alisema. Alisema mradi wa vifaranga vya samaki umepewa kipaumbele cha kwanza kwa ajili ya kuwawezesha wafugaji wa mazao ya baharini kuongeza kipato.

Ufugaji wa majongoo, alisema hivi sasa ni kilimo chenye tija ambacho kitawakomboa wafugaji wa mazao ya baharini kama watajikita na kuweka kipaumbele.

"Tumeanza kuwashajihisha wafugaji wa mazao ya baharini kujikita katika ufugaji wa majongoo ya baharini ambapo soko lake




Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo Zanzibar, Tabia Maulid Mwita, akifungua mafunzo kwa baadhi ya waandishi wa habari, ya kuwajengea uwezo katika kutambua haki za msingi za wanawake ikiwamo kushiriki katika nafasi za uongozi, mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Washawishiwa kuwekeza kisiwani Pemba

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) imesema juhudi zimeanza kuchukuliwa katika kuwashawishi wawekezaji kuwekeza katika kisiwa cha Pemba na kuyatumia maeneo huru ya kiuchumi yaliyotengwa Micheweni Mkoa wa Kaskazini Pemba.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Mudrik Ramadhan Soraga, wakati akijibu swali la Mwakilishi Viti Maalumu Pemba, Bihindi Hamad Khamis, aliyetaka kujua juhudi za serikali kuyatangaza maeneo huru ya uchumi zimefikia wapi.

Alisema Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, tayari ameikitangaza kisiwa cha Pemba kuwa eneo maalumu la uwekezaji kiuchumi.

Uamuzi huo, alisema unakwenda sambamba na kukitangaza kisiwa hicho katika uwekezaji wa miradi mbalimbali ikiwamo hoteli zenye hadhi ya nyota tano.

Aidha, alisema katika mikakati hiyo maeneo huru ya kiuchumi yaliyoko Micheweni Mkoa wa Kaskazini Pemba yatatumika kwa ajili ya uwekezaji wa miradi mbalimbali ya kiuchumi.

"Mheshimiwa Naibu Spika nataka niwajulishe wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba kisiwa cha Pemba hakijatengwa katika uwekezaji. Rais wa Zanzibar amekipa kipaumbele cha kwanza katika uwekezaji wa miradi mbalimbali itakayozalisha ajira," alisema.

Alisema eneo la Micheweni limetangazwa katika mwaka 1992 kuwa maeneo huru ya kiuchumi sambamba na Fumba mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja.

Waziri alisema maeneo hayo ni muhimu na kwa upande wa Micheweni bado eneo hilo halijatumika kikamilifu kwa wawekezaji kuwekeza miradi ya viwanda na kuzalisha ajira.

# Maofisa kilimo, ugani wafundwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAOFISA kilimo na mabwana shamba wametakiwa kuwasimamia wakulima katika maeneo yao, ili kulima kitaalamu na kufikia malengo ya kujitosheleza kiuzalishaji.

Hayo yalisemwa jana mjini Zanzibar na mshauri wa utaalamu wa mipango wa kilimo hai kutoka Wizara ya Kilimo, Omar Abubakar, wakati akifunga mafunzo ya siku tano ya kilimo cha viungo kwa maofisa wa kilimo.

Alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) imeweka kipaumbele katika sekta ya kilimo ili kuwainua wakulima na kuongeza uzalishaji.

Alisema ni wajibu wa wataalamu hao kuhakikisha wanatoa mafunzo bora kwa wakulima ili kuwaingiza katika kilimo cha kisasa na chenye tija kitakachotoa mazao mengi na yenye ubora.

Mazao ya viungo, alisema yana soko kubwa kitaifa na kimataifa, hivyo ni vyema wakulima kuzidisha bidii katika kilimo hicho ili kuwapatia tija.

"Kilimo kizuri cha viungo na chenye soko ni kile kilimo hai ambapo mazao yake huwa ni mazuri zaidi kiafya," alisema.

Alisema Wizara ya Kilimo kupitia mradi wa kilimo cha viungo, imekusudia kuwaorodhesha wakulima hao ili kuhakikisha wananufaika na mipango wa kuwaendeleza kiuchumi.

Kwa upande wao maofisa hao wa kilimo waliiomba Wizara ya Kilimo kufuatilia changamoto zinazowakumba wakulima katika miradi mbalimbali inayoanzishwa ili iwe fursa ya kuzitafutia ufumbuzi na kuanzishwa miradi mipya.

Mafunzo hayo yaliiyotayarishwa kwa pamoja kati ya Wizara ya Kilimo, Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Ofisi ya Zanzibar na People's Development Forum (PDF) yanalenga kuwawapatia wakulima wa viungo mbinu za kisasa za kilimo hicho zitakazowaongezea uzalishaji na kupata masoko ya uhakika.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**NAFASI ZA SHULE**

Keland Nursery and Primary School iliyopo Salasala Rtd inatangaza Nafasi Za Awali Na Msingi. Mawasiliano :0713327613.

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa*

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**LEONARD RAPHAEL MGINA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **LANDROVER DISCOVERY** yenye namba za usajili **T115 BCM** Lenye chases namba **SALLTGM97XA201741** injini namba **10PA2586 KADI** namba 2347775. Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa polisi. Taarifa ya polisi RB. Namba: **IR/TR/RB/208/2021**.

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**JUHUDI ADILI MSOKWA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI YENYE NAMBA ZA USAJILI **MC.980 CSF** AINA YA KINGLION.YEYOTE ATAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU. TAARIFA YA POLISI **MBE/MBE/RB/104257/2021**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**MGAIWE KONDO GILION** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina **TOYOTA CROWN** yenye namba za usajili **T 532 DNF.** Chassis **No. GRS 180 - OO38007**,Engine **NO.4GR - FSE - 0154626.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/ RB/7618/2020.**

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI YA 2)**
**Katika mahakama ya mwanzo DODOMA MJINI**
**Usimamizi wa mirathi 196/2020**
**Ombi la 1. ATHUMANI S. SIMILINGA 2. MUSSA ISSA KUNGA kuteuliwa Msimamizi wa mirathi Marehemu MWAMVITA FARIJALLAH LUPUNGU**

**KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA NA MIRATHI HII TANZANIA BARA.**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe **20/1/2021** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.

Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa.

**Tarehe 16/12/2020**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**Deogratias Alphonce Lyamuya** Mkazi wa Wilaya ya Meatu Mkoani Simiyu atangaza kupoteza kadi yake ya pikipiki aina **Nissan DATSUN** yenye namba za usajili **T923 AMT**,Injini namba SD **23121019** na cheses namba **AGY 720100679.** Taarifa polisi tarehe **12/2/2021** kituo cha polisi kwa RB namba **SIM/MEA/RB/**

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

## Korti yaamuru mume amlipe mke kumtumikia nyumbani

**Beijing,** CHINA

MAHAKAMA ya Talaka ya Beijing, imemuamuru mwanaume kumlipa fidia mke wake, kwa kazi alizomfanyia katika kipindi chote walichooana.

Uamuzi huo ambao ni wa kihistoria unatajwa kuleta mabadiliko katika sheria za China.

Mwanamke huyo atapokea yuan 50,000 sawa na dola 7,700 kwa miaka mitano, aliyofanya kazi za nyumbani bila malipo.

Kesi hiyo iliibua mjadala mkubwa kwenye mitandao ya kijamii, kuhusu thamani ya kazi za nyumbani, huku baadhi wakisema kuwa fidia aliyopewa mwanamke huyo ni kiasi kidogo sana.

Hukumu hiyo inakuja baada ya Uchina kuanzisha sheria mpya zinazohusu jamii.

Kulingana na rekodi za mahakama, mwanaume aliyetambulishwa kwa jina pekee la ubini kama Chen alikuwa amewasilisha kesi ya talaka dhidi ya mkewe kwa jina la ubini Wang, baada ya kuoana mwaka 2015.

Mwanzoni alisita kumtaliki, baadaye aliomba fidia ya pesa, akidai kuwa Chen alikuwa hajafanya kazi yoyote ya nyumbani au kuwajibika vyovyote kwa matunzo ya mtoto wao wa kiume.

Mahakama ya Wilaya ya Fangshan, mjini Beijing, ilimwamrisha kumlipa yuan 2,000 kila mwezi, na malipo ya yuan 50,000 mara moja kwa kazi za nyumbani ambazo alizifanya wakati alipokuwa ameolewa.

Jaji mkuu katika kesi hiyo aliwaambia waandishi wa habari wiki hii kuwa mali za pamoja za wawili hao, walizopata wakati wa ndoa kwa kawaida hugawanywa sawa baina yao.

"Lakini kazi za nyumbani ni mali isiyoweza kuhesabika," alisema jaji.

Hukumu hiyo ilitolewa kulingana na sheria mpya ya makosa ya kiraia, ambayo ilianza kutumika mwaka huu, chini ya sheria hiyo, mke au mume ana haki ya kudai fidia katika talaka, iwapo anafanya majukumu zaidi kwenye malezi ya mtoto, kumtunza ndugu mzee na kumsaidia mke au mume wake kazi.

Awali, wanandoa hao waliotalikiana, wangeweza kuomba aina hiyo ya fidia kama makubaliano kati yao, yangekuwa yamesainiwa na wote wawili, jambo ambalo sio la kawaida kufanyika China.

Katika mitandao ya kijamii, kesi hii iliibua mjadala mkali, huku kampeni katika mtandao wa Weibo iliyotumia alama ya reli ikitazamwa zaidi ya mara milioni 570. **BBC**

# Kenyatta: Mazingira kutatua matatizo kibinadamu

**Nairobi,** KENYA

RAIS wa Kenya, Uhuru Kenyatta akifunga mkutano wa mazingira amesisitiza shida nyingi za mazingira zinazoikabili dunia zinaweza kutoa suluhisho kwa changamoto nyingi tunazokabiliana nazo binadamu.

Mawaziri wa mazingira na viongozi wengine kutoka zaidi ya mataifa 150 walimaliza kikao cha siku mbili kwa njia ya video katika mkutano wa tano wa mazingira wa Umoja wa Mataifa-UNEA-5.

Aidha, katika mkutano huo, bunge lilionya kuwa dunia itakuwa hatarini kwa majanga mapya kama hakuna mabadiliko ya kutunza mazingira ya asili.

**Kadhalika, wanasiasa wa ngazi za juu duniani walisema mabadiliko ya tabianchi ni kitisho kikubwa cha amani.**

Rais wa Kenya, Uhuru Kenyatta alifunga mkutano huo na kusema shida nyingi za mazingira zinaikabili dunia na kwamba, mazingira yanaweza kutoa suluhisho kwa changamoto za binadamu.

Mkutano huo pia ulihudhuriwa na maelfu ya washiriki wa mtandao, wakiwamo zaidi ya wajumbe 1,500 kutoka mataifa ambayo ni wanachama wa Umoja wa Mataifa (UN) na mawaziri zaidi ya 60 wa mazingira.


Bunge ambalo lilionekana moja kwa moja, pia lilikubaliana juu ya mambo muhimu ya kazi za UNEP ikiwamo miaka 50 ya maadhimisho ya UNEP mwakani, kufanya mazungumzo na uongozi kwa wanachama.

Kadhalika, wanasiasa wa ngazi za juu duniani walisema mabadiliko ya tabianchi ni kitisho kikubwa cha amani.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Ujerumani, Heiko Maas, alionya ongezeko la joto duniani, litazidisha mizozo. Maas alitoa wito kwa UN kufanya ulinzi wa mazingira kuwa kipaumbele cha juu.

Waziri Mkuu wa Uingereza, Boris Johnson na Rais wa Ufaransa, Emmanuel Macron pia walitaka kujitolea zaidi kupambana na mabadiliko ya tabianchi.

Johnson alisema mabadiliko ya tabianchi ni kitisho cha usalama wa dunia nzima. **VOA/DW**



Mwili wa Balozi wa Italia, Luca Attanasio, aliyeuawa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), baada ya shambulio dhidi ya msafara wao mjini Goma, ukiwasili mjini Roma, Italia, jana. **PICHA/REUTERS**

# Mwili Balozi Italia wawasili Roma

**Roma,** ITALIA

MWILI wa balozi wa Italia, aliyeuawa nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) katika jaribio la utekaji nyara uliotibuka siku ya Jumatatu, umewasili mjini Roma.

Luca Attanasio, mlinzi wake Vittorio Lacovacci pamoja na dereva raia wa DRC, Moustapha Milambo, waliuawa katika shambulio dhidi ya msafara wa magari ya chakula ya Umoja wa Mataifa (UN), Mashariki mwa nchi hiyo.

Ndege ya kijeshi ya Italia iliyokuwa imebeba majeneza mawili, yaliyokuwa yamefunikwa bendera ya kitaifa ilitua katika uwanja wa ndege wa Ciampino mjini Rome na kupokelewa na Waziri Mkuu, Mario Draghi.

Mamlaka nchini DRC zililaumu kundi la waasi wa Rwanda la FDLR kwa mauaji.

Kundi hilo limekanusha kuhusika na shambulio hilo. **BBC**

## Chama tawala chashinda

**Niamey,** NIGER

MOHAMED Bazoum, mgombea wa Chama tawala cha nchini Niger, Demokrasia na Ujamaa (PNDS-TARAYYA), ameshinda duru ya pili ya uchaguzi wa urais.

Kwa mujibu wa matokeo yaliyotangazwa Jumanne jioni, Niamey na Rais wa Tume Huru ya Kitaifa ya Uchaguzi (CENI), Issaka Souna.

"Idadi ya wapigakura waliopiga kura inakadiriwa kuwa 4,487,195 kati ya wapigakura milioni 7.4 waliojiandikisha, idadi ya waliojitokeza ni asilimia 62.91," alisema Souna.

Matokeo hayo yatapelekwa korti ya kikatiba kwa uthibitisho wa mwisho. **XINHUA**

# GUENDOUZI BADO ANA UTOTO – KOCHA




**LONDON,** England

MATTEO Guendouzi anapitia "ujana" wa soka, kwa mujibu wa Kocha wa Hertha Berlin, Pal Dardai, ambaye anasema mchezaji huyo wa Arsenal ana tabia ya utukutu.

Guendouzi kwa sasa yupo Hertha Berlin akicheza kwa mkopo wa msimu mmoja, baada ya kuhamishwa kutoka kikosi cha kocha Mikel Arteta.

Mfaransa huyo amekuwa akikosolewa mara kwa mara kwa mwenendo wake tangu ajiunge na Washika Bunduki hao mwaka 2018, na Dardai amesema bado yuko mbali na kiwango kinachohitajika cha kukomaa.

Dardai ameliambia gazeti la Bild juu ya maendeleo ya Guendouzi: "Ni kama ujana kwake, yeye ni aina ya watukutu. Lazima afanye kazi na ajifunze kama mnyama."

Katika kipigo cha Jumapili cha mabao 3-0 na RB Leipzig, Guendouzi aliingizwa kama mbadala dakika ya 68 na dakika tatu baadaye, alipoteza mpira ndani ya sanduku la penalti, na kusababisha bao la pili la Leipzig.

Guendouzi amekuwa akipangwa katika kikosi cha kwanza cha Hertha, akicheza mechi 17 kwenye mashindano yote hadi sasa.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 amefunga mabao mawili na kutoa asisti moja katika kipindi hicho, na kupata sifa maalum kutoka kwa mkurugenzi wa michezo wa klabu hiyo, Arne Friedrich.

"Ni mchezaji mzuri," alisema Friedrich. "Tunafurahi sana kuwa naye hapa na ana thamani ya kila senti."

# Pirlo: Juve inaweza kutwaa ubingwa

**TURIN,** Italia

KOCHA wa Juventus, Andrea Pirlo ana matumaini makubwa ya kuiongoza timu hiyo, kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Italia, Serie A, kwa kuahidi kwamba watapambana hadi mwisho dhidi ya Inter Milan na AC Milan.

Usiku wa Jumatatu, Juventus iliibuka na ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Crotone na Cristiano Ronaldo ndio alikuwa shujaa baada ya kufunga mabao mawili na kuisaidia timu hiyo kusogea hadi nafasi ya tatu kwenye msimamo.

Juventus wamepitwa pointi nane na Inter Milan ambao ndio vinara wa Ligi Kuu Italia wakiwa na pointi 53.

"Tulianza kuwa na wasiwasi kidogo, labda baada ya kufungwa mchezo wetu wa mwisho," amesema Pirlo akiwaambia waandishi wa habari.

Kwa sasa Inter Milan wanaonekana kutawala mbio za ubingwa wa Serie A baada ya kuitwanga AC Milan 3-0 mwishoni mwa wiki.





# *Silva kumrithi Cavani Utd*

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United inapanga kumsajili mshambuliaji wa Eintracht Frankfurt, Andre Silva katika kipindi kinachokuja cha majira ya joto, kwa mujibu wa Daily Mail.

Usajili wa Silva utafanyika tu iwapo Edinson Cavani hataongeza muda wake wa kukaa pale Old Trafford, kwa mujibu wa ripoti.

Cavani amekuwa akifanya vizuri sana kwa muda mfupi aliokuwapo Old Trafford na mkataba wake una chaguo la kuongeza mwaka mwingine. Taarifa zinaonyesha United wana mpango wa kumbakiza hapo ili aendelee kuwa naye kwenye vitabu vyao kwa msimu ujao wa 2021-22 licha ya umri wake na kuumia kwa hivi karibuni.

Mashetani Wekundu wanatarajiwa wataingia sokoni kwa ajili ya nyota huyo mpya msimu huu wa joto bila kujali, wakati Erling Braut Haaland akihusishwa na dili la mabadilishano la kwenda upande Manchester City.

## HABARI MICHEZO

# Klopp aendelea kuweweseka

**LIVERPOOL,** England

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp amedai kuwa kikosi chake kingekuwa karibu na viongozi wa Ligi Kuu England, Manchester City msimu wa 2020-21 ungekuwa wa kawaida.

Wachezaji kadhaa muhimu wa Liverpool wameumia, haswa katika safu ya ulinzi ambapo Virgil van Dijk, Joe Gomez na Joel Matip wote wanaweza kukosa kipindi chote kilichobaki cha msimu huu.

Kikosi cha Klopp kilishinda taji lao la kwanza la Ligi Kuu England msimu uliopita kwa kipindi cha miaka 30, lakini kwa sasa wanajikuta katika nafasi ya sita, alama 16 nyuma ya kikosi cha City cha kocha, Pep Guardiola.

"Kwa hilo tunahitaji bahati zaidi, kwa kweli. Bahati zaidi na majeruhi na tunaweza kukaribia nafasi hiyo.

"Sote tunakubali, na nina hakika Pep angesema kwamba, katika msimu wa kawaida kwa timu zote mbili hatutakuwa na alama 16 ugenini.

"Lakini tuko hivyo. Ndivyo ilivyo. Tunakubali. Msimu huu sio wasiwasi wetu jinsi tunavyokaribia City. Ni umbali gani tunaweza kupanda. Hiyo ni kazi ya kutosha kufanya," aliongeza Klopp.



# HAALAND ASHAURIWA KUONDOKA BUNDESLIGA



**MUNICH,** Ujerumani

NYOTA wa Borussia Dortmund, Erling Haaland anapaswa kujiunga na Bayern Munich au aondoke kwenye Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, ili kuendeleza kipaji chake, mkongwe Lothar Matthaus.

Mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Norway alifunga mara mbili katika ushindi wa 4-0 dhidi ya Schalke wikendi iliyopita na kufikisha mabao 27 katika mashindano yote msimu huu, nyuma ya Robert Lewandowski (31) kati ya wachezaji wa Bundesliga.

Haaland pia ilifunga mara mbili katika ushindi wa 3-2 dhidi ya Sevilla kwenye mchezo wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa hatua ya 16 na kuwa mchezaji wa kwanza katika historia ya mashindano hayo kufunga mabao 17 katika mechi 13 za kwanza.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20 alijiunga na Dortmund Januari, mwaka huu, lakini tayari anahusishwa na kuwaniwa na klabu kubwa Ulaya.

Real Madrid, Barcelona, Manchester United, Manchester City na Chelsea zote zimetajwa kumhitaji Haaland, ambayo inakisiwa kuwa na kifungu cha kutolewa cha euro milioni 75, ambayo itaanza kutumika mwaka 2022.

"Katika umri mdogo, yeye ni mshambuliaji tofauti na yoyote ambayo nimewahi kuona hapo awali, hesabu ya malengo haya, nguvu hii, shauku, nguvu, na ubora pia," amesema Matthaus aliiambia Sport1.

# *Arteta: Arsenal tatizo umaliziaji*

**LONDON,** England


KOCHA Mkuu wa Arsenal, Mikel Arteta amesema kuwa tatizo kubwa ambalo linaikumba timu yake ni umaliziaji wa nafasi ambazo wanazitengeneza ndani ya uwanja.

Kwa sasa Arsenal inajiandaa na mchezo wao wa leo wa hatua ya 32 bora dhidi ya Benfica kwenye Ligi ya Europa.

Ikiwa Uwanja wa Emirates, Februari 21, mwaka huu iliruhusu kichapo cha bao 1-0 dhidi ya Manchester City kwenye mchezo wa Ligi Kuu England.

Arteta amesema: "Tatizo kubwa kwa timu kwa sasa lipo kwenye umaliziaji kwani wamekuwa wakitengeneza nafasi nyingi na kushindwa kuzitumia ndani ya uwanja.

Arsenal watacheza nchini Ugiriki katika Jiji la Athens wakiwa nyumbani baada ya Taifa la England kukataa mechi hiyo isipigwe nchini kwao kutokana na kuamini kwamba Ureno kuna corona nyingi, hivyo wachezaji wa Benfica wangekwenda kuliongeza janga hilo.



## KWA UFUPI

### DYBALA NJIA PANDA

HATIMA ya mshambuliaji wa Argentina, Paulo Dybala kuendelea kuwachezea mabingwa wa Ligi Kuu Italia, Serie A, Juventus haijulikani na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 anaweza kuuzwa msimu huu. (**Mirror**)

### UNITED, SPURS VITANI

KLABU za Liverpool, Manchester United na Tottenham ni miongoni mwa timu zinazomwania mshambuliaji wa Juventus, Paulo Dybala mwenye umri wa miaka 27 na raia wa Argentina. (**Goal**)

### HENDERSON AGOMBEWA

TOTTENHAM na Borussia Dortmund zinaongoza katika mbio za kumsajili mlinda mlango wa Manchester United, Dean Henderson mwenye umri wa miaka 23. (**Sky Sports**)

### CHELSEA YAMFUATA HAALAND

CHELSEA inaamini itamsajili mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Norway, Erling Braut Haaland mwenye umri wa miaka 20 kutoka Borussia Dortmund kipindi cha majira ya joto. (**Eurosport**)

### ABRAMOVICH KUMWAGA FEDHA

MMILIKI wa Chelsea, Roman Abramovich atampa kocha wake, Thomas Tuchel kiasi cha pauni milioni 260 kwa ajili ya usajili wa dirisha la kipindi cha majira ya joto, bila kujalli kama klabu itafuzu kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya. (**Tutto Mercato, via Star**)

### WEST KUMUUZA RICE

KLABU ya West Ham itasikiliza ofa iliyozidi pauni milioni 100 ili kumwachia kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya England, Declan Rice mwenye umri wa miaka 22. (**Talksport**)

### SILVA ANUKIA UNITED

KLABU ya Manchester United inaweza kupatiwa nafasi ya kumsajili mshambuliaji wa Eintracht Frankfurt, Andre Silva mwenye umri wa miaka 25, wakati wa dirisha la usajili msimu wa joto. (**Sun**)

### BADIASHILE SOKONI

KOHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer anamfuatilia mlinzi wa kimataifa wa Monaco, Benoit Badiashile mwenye umri wa miaka 19. (**Mirror**)

### MILENKOVIC AWINDWA

MLINZI wa kati wa Fiorentina, Mserbia Nikola Milenkovic mwenye umri wa miaka 23, ni chaguo namba moja anayewaniwa na Borussia Dortmund. (**Sky Sports German**)

### ARSENAL KUMUUZA NELSON


ARSENAL itasikiliza ofa kwa ajili ya kiungo wa kati, Reiss Nelson mwenye umri wa miaka 21, mwishoni mwa msimu huu. (**CBS, via Mirror**)

### AZEEZ MAMBO SAFI

ARSENAL ipo kwenye mazungumzo na mchezaji wao kinda, Miguel Azeez mwenye umri wa miaka 18, kuhusu kuongeza mkataba wa muda mrefu. (**Sun**)



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# ODEGAARD ATAKIWA ASIONDOKE ARSENAL

●●●Kiwango cha kiungo huyo kinatajwa kuwa ni faida kubwa, huku Madrid ikionyesha nia ya kumrejesha...

**LONDON,** England

KIUNGO wa Arsenal na Timu ya Taifa ya Ghana, Thomas Partey amesema anafuraha kucheza na Martin Odegaard katika eneo la kiungo.

Odegaard mwenye umri wa miaka 22, raia wa Norway alisajiliwa Arsenal wakati wa dirisha dogo la Januari, mwaka huu akitokea Real Madrid kwa mkopo baada ya kukosa nafasi ya kucheza katika kikosi cha kwanza.

Licha ya Odegaard kutocheza mechi nyingi za kubainisha kiwango chake akiwa na wababe hao, lakini Partey mwenye umri wa miaka 27, amesema ni faida kubwa kuwa naye kwenye timu.

Amesema anakubali staili ya uchezaji na vitu alivyonavyo kiungo huyo akikumbuka jinsi alivyokuwa akipata wakati mgumu anapokabiliana naye kwenye mechi za Ligi Kuu Hispania, La-Liga, wakati Odegaard akiwa Real Sociedad kwa mkopo na yeye akiwa Atletico Madrid.

"Ni ngumu sana kucheza dhidi yake. Nakumbuka kucheza dhidi yake ni mjanja sana mara zote ni mwepesi akiwa na mpira hakupi nafasi ya kuupata," alisema Partey akinukuliwa na Sky Sport.

"Inafurahisha kuwa naye hapa, nina imani atakuwa na msimu mzuri na atatusaidia kufanikisha kile tunachotaka."

Odegaard alijiunga na Real Madrid mwaka 2015 akitokea klabu ya Stromsgodset akiwa na umri wa miaka 16 akionekana kama moja ya makinda chipukizi wenye kipaji kikubwa cha kucheza mpira katika ulimwengu wa soka.

Lakini mambo hayakwenda sawa huko Madrid kwani hakupata nafasi ya kucheza hali iliyosababisha atolewe kwa mkopo kwenda Heerenveen, Vitesse, Real Sociedad na sasa Arsenal.

***

## HABARI MICHEZO

# SIMBA IMEITENDEA HAKI VISIT TANZANIA

**Na Somoe Ng'itu**

WAZIRI wa Utalii na Maliasili, Dk. Damas Ndumaro, amesema Simba imeitendea haki kwa kiwango cha juu jezi yao yenye ujumbe wa 'Visit Tanzania' katika mechi zake za hatua ya makundi ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Simba iliingia makubaliano na serikali kwa kuvaa jezi yenye ujumbe huo kwenye mechi zake baada ya mdhamini wake Sportpesa kukinzana na mdhamini mwingine wa Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Ndumbaro ametoa kauli hiyo baada ya Simba kupata ushindi mara mbili mfululizo, ugenini dhidi ya AS Vita ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), na Al Ahly iliyochezwa juzi kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

**Wawakilishi hao wa Tanzania maarufu Wekundu wa Msimbazi walipata ushindi wa bao 1-0 Mjini Kinshasa, DRC juzi wakapata tena ushindi kama huo dhidi ya vigogo wa Afrika kutoka Misri.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Ndumbaro alisema wataendelea kushirikiana na Simba kuhakikisha wanapeperusha vyema bendera ya Tanzania katika mashindano hayo yanaendelea barani Afrika.

Waziri huyo alisema pia watahakikisha michezo yote inafanya vyema katika mashindano ya kimataifa na kuendelea kutangaza jina la Tanzania vizuri.

"Tunaipongeza sana Simba kwa kazi nzuri waliyofanya, kiukweli wameitendea haki zaidi Visit Tanzania katika mechi zote mbili walizocheza, tutahakikisha wanaendelea kufanya vizuri kwenye michezo inayofuata, na hii haitaishia kwa Simba tu, tunataka kuona michezo yote inafanya vizuri katika mashindano ya kimataifa," Ndumbaro alisema.

Simba yenye pointi sita ndio inaongoza katika msimamo wa Kundi A ikifuatiwa na Al Ahly yenye pointi tatu sawa na AS Vita huku Al Merrikh ambayo imepoteza mechi zake mbili ilizocheza ikiburuza mkia kwenye kundi hilo.

Baada ya mechi hiyo ya juzi, Simba sasa itasafiri kuelekea Khartoum, Sudan kuwafuata Al Merrikh kati ya Machi 5 na 6, mwaka huu halafu itarejea nyumbani kuwasubiri Wasudani hao.

Mechi itakayofuata itachezwa mapema Aprili kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa dhidi ya AS Vita na itamalizia hatua ya makundi nchini Misri dhidi ya Al Ahly.




Mashabiki wa Simba wakiingia kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, huku wakicheza 'kigoma' kwa ajili ya kutazama mechi ya Kundi A ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Al Ahly kutoka Misri. Simba ilishinda bao 1-0. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Bashungwa mgeni Kili Marathon

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Innocent Bashungwa, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika mbio za mwaka huu za Kilimanjaro Marathon zitakazofanyika keshokutwa Moshi, mkoani Kilimanjaro.

Kwa mujibu wa waandaaji wa mbio hizo, Bashungwa amethibitisha kushiriki na ataongozana na viongozi wengine wa mkoa, Chama cha Riadha Tanzania (RT), Chama cha Riadha Mkoa wa Kilimanjaro na wadau wengine wa mchezo huo.

Hii itakuwa ni mara ya kwanza kwa Bashungwa kuwa mgeni rasmi katika mashindano hayo kama waziri mpya wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Taarifa zaidi zinasema maandalizi yote yamekamilika na tayari namba za ushiriki zimeshatolewa kwa mikoa ya Dar es Salaam na Arusha huku mchakato huo kwa mji wa Moshi unatarajiwa kufanyika leo kuanzia saa sita mchana hadi keshokutwa.

## *Senzo afunguka kuhusu Mosimane*

**Na Adam Fungamwango**

MSHAURI wa masuala ya mabadiliko wa Yanga, Senzo Mbatha, amesema hakuwa na mpango wowote wa kuihujumu Simba kama ilivyotafsiriwa na baadhi ya watu baada ya kuonekana akifanya mazungumzo na Kocha Mkuu wa Al Ahly, Pitso Mosimane.

Senzo alisema hayo kufuatia Mkuu wa Idara ya Habari wa Mawasiliano wa Simba, Haji Manara, kumlalamikia kwa kitendo chake cha kwenda kuonana na kocha huyo siku moja kabla ya Wekundu wa Msimbazi kuwavaa Al Ahly.

Kiongozi huyo alisema aliamua kwenda kukutana na Mosimane kwa sababu ni 'swahiba' wake kwa sababu hawajaonana kwa muda mrefu.

Katika mitandao ya kijamii zilivuja picha zinazoonyesha Senzo ambaye alikuwa Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba akiwa na Mosimane ambao wote ni raia wa Afrika Kusini, wakifanya mazoezi.

"Hakukuwa na siku nyingine ambayo ningeweza kwenda kuonana naye zaidi ya Jumatatu. Nisingeweza kuonana naye siku ya Jumanne kwa sababu walikuwa na ratiba ya kusafiri," alisema Senzo.

Alisema kuwa hana kitu cha kumwambia kocha huyo ambaye yeye hakijui, na badala yake alikwenda kuonana naye kama rafiki yake, kusalimia na wakanywa naye kahawa.

"Kitu gani ambacho naweza kumwambia Mosimane ambacho yeye hajui? Kwa kifupi, nilikutana na rafiki yangu ambaye sijaonana naye muda mrefu. Nilionana naye sehemu ya wazi ambayo kila mtu anaona na nilikunywa naye kikombe cha kahawa. Lakini naelewa niko kwenye ulimwengu wa Tanzania," Senzo alisema.

## Riadha kwenda kujifua Nairobi

**Na Shufaa Lyimo**

TIMU ya taifa ya riadha itakayoshiriki mashindano ya Olimpiki inatarajia kwenda jijini Nairobi nchini Kenya wiki ijayo kwa ajili ya kujiandaa na michuano hiyo, imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kaimu Katibu Mkuu wa Chama cha Riadha Tanzania (RT), Ombeni Zavalla, alisema maandalizi ya kambi hiyo yanaendelea na wanaamini itasaidia kuwajenga wanamichezo wao.

Zavalla alisema awali walipanga kambi hiyo ianze mapema, lakini ukata unaowakabili umesababisha kuanza mapema.

"Wachezaji ambao wanajiandaa na mashindano ya Olimpiki wanatarajiwa kuingia kambini mwishoni mwa mwezi huu, na tumechagua kambi yao itakuwa Nairobi, tunaamini ni mahali sahihi kwao kujinoa," alisema Zavalla.

# Michezo

Alhamisi Februari 25, 2021

Nipashe




Odegaard atakiwa asiondoke Arsenal UKURASA 22




Beki wa Simba, Shomary Kapombe (kushoto), akiwania mpira dhidi ya mchezaji wa Al Ahly ya Misri katika mechi ya Kundi A ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam juzi. Simba ilishinda bao 1-0. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Yanga kuikabili Kengold kibabe

**Na Saada Akida**

ILI kuhakikisha timu yao inasonga mbele, mabosi wa Yanga wamesema tayari wamepata taarifa muhimu za 'kuwamaliza' wapinzani wao katika mechi ya mzunguko wanne wa mashindano ya Kombe la FA, Kengold FC ya jijini Mbeya.

Yanga itawakaribisha Kengold katika mechi ya michuano hiyo itakayochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa Uhuru.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Thabit Kandoro alisema mchakato wa kuipeleleza Kengold ulianza mapema baada ya ratiba kutolewa na walimpatia taarifa hizo za kiufundi kocha wao, Cedric Kaze.

"Hatutadharau timu yoyote ambayo tunakutana nayo, Kengold FC sio timu ya kuibeza, tumewafuatilia na taarifa zao tumeziwasilisha kwenye benchi la ufundi ili kufanyiwa kazi," alisema Kandoro.

## Namungo FC, De Agosto kazini

**Na Mwandishi Wetu**

TIMU ya Namungo FC inatarajia kuwakaribisha CD Primiero de Agosto kutoka Angola katika mechi ya marudiano ya mtoano ya michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Azam Complex jijini Dar es Salaam.

Namungo itashuka katika mchezo huo ikiwa na kumbukumbu ya ushindi wa mabao 6-2 walioupata katika mechi ya kwanza iliyochezwa Jumapili iliyopita.

Kocha Mkuu wa Namungo FC, Hemedi Morocco alisema wamejipanga kusaka ushindi katika mechi ya leo na kamwe hawajabweteka na matokeo ya mechi ya kwanza.

Morocco alisema licha ya kucheza katika ardhi ya nyumbani, bado anaimani mechi hiyo itakuwa na ushindani kwa sababu wapinzani wao wanaweza kubadilika kutokana na kutohitaji 'kugeuza' matokeo.

Mshindi wa jumla wa mechi hiyo ataingia kwenye hatua ya makundi na tayari ratiba inaonyesha amepangwa Kundi D lenye timu za Raja Casablaca ya Morocco, Pyraminds (Misri) na Nkana ya Zambia.

# Simba: Tulistahili ushindi

**Na Saada Akida**

### ●●● Mfaransa asema nidhamu ya wachezaji iliwabeba huku Al Ahly wakilalamika joto...

WAMEKAA! Kocha Mkuu wa Simba, Didier Gomes, amesema kikosi chake kilistahili kupata ushindi katika mechi ya Kundi A ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Al Ahly kutoka Misri kwa sababu wachezaji wake walicheza mpira kwa nidhamu ya hali ya juu.

**Simba ilipata ushindi wa bao 1-0 na kufikisha pointi sita ambazo zimewafanya wawe vinara katika Kundi A wakifuatiwa na AS Vita ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Al Ahly na Al Merrikh ya Sudan ambayo haina pointi inaburuza mkia.**

Gomes aliliambia gazeti hili nidhamu hiyo ya mechi iliwasaidia kupata matokeo chanya katika mchezo huo wa pili katika hatua ya makundi ya michuano hiyo inayosimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Mfaransa huyo alisema ameridhishwa na uwezo walioonyesha wachezaji wake katika mchezo huo na namna walivyopambana kulinda bao ambalo walilipata kupitia Luis Miquissone.

"Nimefurahi kupata ushindi wa bao 1-0, matokeo haya tumeweza kuongeza pointi na sasa kuwa na alama sita, hii ni ishara nzuri kwetu, kuelekea mechi zetu zijazo tunaamini pia zitakuwa ngumu na zenye ushindani mkubwa," alisema Gomes.

Kocha huyo pia aliwapongeza wachezaji wake kufanya kile alichowaelekeza licha ya kuwapo kwa changamoto mbalimbali katika mchezo huo, lakini muhimu walifanikiwa kila mmoja kutimiza majukumu yake ambayo aliwapa wakiwa kwenye mazoezi.

Naye Kocha Mkuu wa Al Ahly, Pitso Mosimane, aliipongeza Simba kwa ushindi waliopata na kusema anaamini hawajafungwa kwa kuzidiwa mbinu bali hali ya hewa ya joto haikuwa rafiki kwa wachezaji wake. Mosimane alisema walijitahidi namna ya kucheza na wapinzani wao, lakini ilishindikana kwa sababu ya changamoto hiyo ya hali ya hewa.

"Tulicheza mpira mzuri, tulijitahidi kwenda na wapinzani wetu na hili tulijua tangu awali jambo ambalo lilitufanya nasi tuongeze juhudi ndani ya uwanja, hatujapoteza kimbinu ila hali ya hewa muda wa jioni haikuwa rafiki, hivyo tumejitahidi na tukashindwa kupata matokeo."

"Simba wanapaswa wapewe pongezi kwa kutumia vizuri upungufu wetu ila hatujapoteza na bado tuna kazi mbele, hatujakata tamaa tunaenda kujipanga kwa dakika 90 zijazo," Mosimane.

Mechi inayofuata ya Simba itachezwa kati ya Machi 5 na 6, mwaka huu, jijini Khartoum dhidi ya wenyeji Al Merrikh na baadaye itarudi nyumbani kuwasubiri Wasudan hao ambao wanaburuza mkia.

Wakati huo huo, shangwe zilizoonyeshwa na mashabiki wa Simba zimewavutia mabosi wa Mamelodi Sundowns ambao wameomba sapoti katika mchezo wao wa Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya CR Belouizdad ya Algeria itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >